




**Shehena** mafuta ya kula yanaswa ikisafirishwa kwa jahazi baharini

UKURASA 3




UKURASA 9

Nipashe JUMAPILI
Jumapili Novemba 27, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581142
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Watumishi warejesha mamilioni waliyofuja

• **Baadhi** watiwa mbaroni na polisi...*Ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### RAIS: BURUNDI IMEIPOKEA CRDB

RAIS wa Jamhuri ya Burundi, Evariste Ndayishimiye ameipongeza Benki ya CRDB Burundi kwa mafanikio makubwa iliyopata katika kipindi cha miaka 10 ya kuwapo kwake Burundi na kusema kuwa nchi hiyo imeipokea benki hiyo kwa mikono miwili na inajivunia kuwapo kwake nchini humo...

UKURASA WA 18

### VIGOGO WA CHADEMA WAPAA ULAYA KIMKAKATI

VIONGOZI waandamizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wako ziarani barani Ulaya kwa siku saba kwa lengo la kutafuta uungwaji mkono katika jumuiya za kimataifa kuimarisha demokrasia nchini...



Rais Samia Suluhu Hassan, akikabidhi zawadi kwa mmoja wa maofisa wanafunzi waliofanya vizuri kwenye masomo yao, kabla ya kutunuku kamisheni kwa maofisa hao 724, wakati wa sherehe katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli, mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**

## Samia atunuku kamisheni maofisa wapya

UKURASA 2



## Spika Tulia aonya utendaji UVCCM

UK. 4

MICHEZO **SIMBA HASIRA ZOTE KWA POLISI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Dereva wa pikipiki yenye namba za usajili MC 614 DLM, akivunja sheria za usalama barabarani kwa kuwapakia watoto wadogo chini ya miaka mitano katika eneo la Buza, mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watumishi warudisha mamilioni waliyoyafuja

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

WATUMISHI wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba mkoani Singida wamerejesha Sh. milioni 136.1 kati ya Sh. milioni 339.6 wanazodaiwa za mapato walizokusanya na kuzitumia badala ya kuzipeleka benki kwenye akaunti ya halmashauri.

Wadaiwa hao wamerejesha fedha hizo katika akaunti za Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ambazo walizikusanya kupitia mashine ya kukusanyia mapato baada ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba kusimamia kidete urejeshaji wa fedha hizo. Serukamba katika kikao na watumishi hao jana akiwa amefuatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, aliwataka wadaiwa hao kuwasilisha risiti za malipo benki au fedha taslimu kwa wahasibu waliokuwapo ukumbini.

Baada ya mahojiano ya muda mrefu kwa kila mdaiwa, ilibainika wengi wao walikwishalipa lakini stakabadhi za benki walikuwa hawajaziwasilisha kwa wahasibu wa halmashauri hiyo.

Serukamba alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomora kusimamia kikamilifu Idara ya Uhasibu ambayo ilionekana kutotekeleza wajibu wake katika kufuatilia wadaiwa hao.

Mkuu wa mkoa huyo pia aliagiza kuanzia sasa kila mwenye mashine ya kukusanya mapato ya serikali awe anapeleka benki fedha alizokusanya badala ya kukaa nazo, jambo linatoa vishawishi kuzitumia na kujikuta wamelimbikiza madeni.

Serukamba alisema kuwapo wadaiwa sugu kumetokana na wahasibu kutofuatilia pindi wanapogawa mashine za kukusanya fedha na wakati mwingine kutohakiki madeni ya risiti wanazopatiwa na wadaiwa hao.

Pia aliagiza kupatiwa taarifa za makusanyo kila baada ya siku mbili na zionyeshe kiwango cha madeni kilichokusanywa pamoja na makusanyo mapya. Baadhi ya wadaiwa wakati wakihojiwa, waliahidi kulipa fedha hizo zilizobaki katika kipindi cha wiki mbili hadi miezi mitatu ijayo huku wengine wakiishia mikononi mwa polisi.

Serukamba aliwataka wasimamizi wa mfumo wa fedha katika halmashauri hiyo kuhakikisha wanahakiki madeni ndani ya mfumo ambayo yameshalipwa na kuyafuta ili yabaki madeni halisi.

Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda alitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuwa kutokana na ufujaji wa fedha hizo, watumishi sita akiwamo Ofisa Biashara wa Wilaya ya Iramba na Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya hiyo (DT) walifukuzwa kazi baada ya kubainika wamehusika katika ubadhirifu wa mamilioni ya shilingi yatokanayo na makusanyo ya mapato.

Alisema watumishi waliofukuzwa kazi ni kati ya 72 waliofikishwa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhojiwa baada ya kubainika walizikusanya fedha hizo kutoka kwa wananchi lakini badala ya kuzipeleka benki kwenye akaunti za halmashauri wakaamua kuziweka mifukoni mwao.

"Agosti 3 mwaka huu Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya Iramba lilikutana na kujiridhisha kuwa watumishi sita walikusanya fedha wakazitumia, hivyo likaazimia kuwafuta kazi akiwamo Ofisa Biashara wa Wilaya, Prosper Banzi na Mweka Hazina wa Halmashauri, Mwidin Mohammed," alisema.

Hatua zilianza kuchukuliwa haraka baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kutoa maagizo alipofanya ziara Julai 16 mwaka huu wilayani Iramba.

# Samia atunuku kamisheni kwa maofisa wapya 724

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu amewatunuku kamisheni maofisa wapya 724 wa Luteni Usu wakiwamo 109 wa Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Kijeshi katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (TMA) mkoani Arusha.

Kabla ya kutunuku kamisheni jana, Rais Samia alikagua gwaride lililoandaliwa na maofisa hao ambao kijinsia ni wanaume 651 na wanawake 89.

Wengine 16 ni kutoka nchi rafiki za Kenya (2), Uganda (2), Burundi (2), Eswatini (8) na Rwanda (2) ambao watatunukiwa katika nchi zao huku watanzania 20 wakipata mafunzo yao toka nchi rafiki za China (5), India (2), Kenya (5) na Urusi (5).

Kabla ya kuwatunuku kamisheni maofisa hao, Rais Samia aliwapongeza kwa kuhitimu na kutoa zawadi kwa baadhi yao waliofanya vizuri zaidi katika medani mbalimbali.

Waliopewa zawadi ni Baraka Yusuph aliyefanya vizuri zaidi kwenye Shahada ya Sayansi ya Kijeshi, huku Joseph Muovela akifanya vizuri kwenye medani wakati Japhet Mshana na Catherine Kastori wamefanya vizuri zaidi darasani.

Wengine waliopewa zawadi kutoka kundi la 69/2021 ni Robert Masaga aliyefanya vizuri zaidi, Julius Kahabi (medali), Rajabu Ramadhani Ismail na Fatuma Makung'uto Makung'uto kwa kufanya vizuri darasani, huku Christopher Muriuki kutoka Kenya naye akifanya vizuri zaidi.

Baada ya kuwatunuku Kamisheni na Shahada ya Sayansi ya Kijeshi, Rais Samia alivunja mahafali ya tatu ya Shahada ya Sayansi ya Kijeshi kati ya Chuo cha TMA na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

Awali Mkuu wa Chuo cha Kijeshi Monduli (TMA), Brigedia Jenerali Jackson Mwaseba alisema maofisa hao ni kutoka kundi cha tatu la mwaka 2019 la Shahada ya Sayansi ya kijeshi na kundi la 69 la mwaka 2021.

"Katika kundi hili la Shahada ya sayansi ya kijeshi walianza mafunzo yao Novemba 6 mwaka 2019 wakiwa maofisa wanafunzi 119 lakini kutokana na makosa mbalimbali 10 walifukuzwa kozi na hadi leo wametunukiwa maofisa wapya 109," alisema.

Brigedia Jenerali Mwaseba alisema katika kundi la pili la kozi ya 69/2021 maofisa wanafunzi 1,029 walianza kozi Oktoba 4 mwaka 2021 na kati yao 415 walifukuzwa kutokana na makosa mbalimbali na waliotunukiwa kamisheni ni 595 katika kundi la 69 la mwaka 2021, huku 10 walifukuzwa katika kundi la tatu la mwaka 2019 la shahada ya sayansi.

Alitaja baadhi ya makosa yaliyosababisha kutofikia siku hiyo ni pamoja na utovu wa nidhamu, ugonjwa, vifo na kukimbia mafunzo.

# Wahitimu wapewa angalizo rushwa na dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Hamadi Hassan Chande amewataka wahitimu wa vyuo mbalimbali nchini wakiwamo wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), kufanya kazi kwa ubunifu, uaminifu na uadilifu na kujiepusha na vitendo vya rushwa, ufisadi, wizi na matumizi ya dawa ya kulevya.

Alitoa angalizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mahafali ya 48 ya IFM katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam ambako zaidi ya wahitimu 4,000 walitunukiwa tuzo mbalimbali.

Alisema IFM imekuwa mstari wa mbele katika kuongeza idadi ya watanzania wenye taaluma na utaalamu katika Sekta ya Fedha, Uhasibu, Bima na Hifadhi za Jamii, hivyo ni vyema idadi hiyo iendane na kukidhi mahitaji ya soko ambayo yanahitaji wanataaluma wenye weledi na uadilifu.

Chande pia aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa kuzalisha wataalamu katika fani mbalimbali na kuliwezesha taifa kufikia malengo yake ya kujitosheleza katika fani za fedha kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi, kiteknolojia, kisiasa na kijamii.

Kwa upande wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, Chande alisema serikali itaendelea kuongeza kiwango cha wanafunzi wanaopata mikopo mwaka hadi mwaka ili wanafunzi wenye sifa wanufaike. Alisema jambo hilo litawezekana endapo wale wote waliopata mkopo wa serikali kwa ajili ya kuwasaidia kuweza kutimiza ndoto zao, watarejesha mikopo waliyopata kwa wakati hivyo kuiongezea serikali uwezo wa kutoa fursa za mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi.

Katika mahafali hayo, Kaimu Mkuu wa IFM, Dk. Imanueli Mnzava alisema chuo kimeendelea kurahisisha upatikanaji wa mafunzo kwa wananchi kwa kusogeza huduma za mafunzo hayo karibu na wahitaji.

"Chuo kina kampasi Mwanza, Dodoma, Simiyu na sasa tunamalizia ujenzi Kampasi ya Geita kwa ufadhili wa serikali. Kama tunavyofahamu elimu ni chachu ya mabadiliko ya kitabia, kiutendaji na uwezo wa kubadilisha mazingira yanayotuzunguka," alisema Dk. Mnzava.

Aliongeza kuwa licha ya mafanikio mbalimbali yaliyopatikana chuoni hapo, wanakabiliwa na uhaba wa madarasa, ofisi na mabweni ya wanafunzi, hivyo kuiomba serikali isaidie kupata majengo yaliyo karibu na chuo ili kurahisisha utoaji wa elimu bora kulingana na mahitaji ya soko.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la Chuo, Prof. Emanuel Mjema alisema wataendelea kusimamia utekelezaji wa malengo ya chuo na kuainisha vipaumbele kwa kuzingatia misingi ya tija na upatikanaji rasilimali ili kuboresha viwango vya wahitimu watakaojiajiri na kujitegemea na pia kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Chuo hicho kilianzishwa mwaka 1972 kikiwa na uwezo wa kutoa kozi mbili, ambapo jumla ya wahitimu 59 walihitimu mwaka huo. Chuo hicho kwa sasa kinatoa zaidi ya kozi 33 katika fani mbalimbali zikiwamo Fedha, Bima na Uhasibu.

## HABARI KITAIFA

# Mimba za utotoni zashtua

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amekerwa na kukithiri mimba za utotoni wilayani Ukerewe na kuwataka wananchi wilayani humo kuhakikisha wanapinga na kukomesha vitendo hivyo ili kuwanusuru watoto wa kike wanaonyimwa haki yao ya kupata elimu.

Dk. Mpango aliagiza hayo jana katika Kata ya Igalla wilayani Ukerewe mkoani Mwanza alipozindua Kituo cha Afya kilichogharimu Sh. milioni 492.37 baada ya kupokea taarifa ya mkoa huo iliyoonyesha wilaya hiyo ina idadi kubwa ya watoto wanaopata ujauzito na kulazimika kuacha shule.

"Watoto wa kike wanapopata mimba za utotoni wanakuwa wako katika hatari kubwa ya kupata magonjwa ya kudumu , hivyo kusababisha taifa kukosa nguvu kazi na viongozi bora wa baadaye," alitahadharisha.

Makamu wa Rais aliwataka wazazi, walezi na jamii kuwa walinzi wa watoto ikiwa ni pamoja na kuacha tabia ya kuwaozesha mabinti wakiwa na umri mdogo.

Dk. Mpango pia aliagiza ifikapo Februari mwakani, Kituo cha Afya Igalla kiwe kimeanza kutoa huduma kikiwa na madaktari na vifaa tiba.

Jetruda Masubi ni mkazi wa Kata ya Igalla anayeshuhudia kuwa kabla ya kituo hicho cha afya kujengwa, walikuwa wakipata adha hususani wanawake wajawazito waliokuwa wanalazimika kusafirishwa umbali mrefu kupata huduma huku baadhi yao wakijifungua njia na wengine kupoteza maisha kutokana na kukosa huduma za dharura.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Dk. Getera Nyangi alisema ujenzi wa Kituo cha Afya Igalla utasaidia kupunguza gharama za usafiri kwa wananchi waliokuwa wakifuata huduma za afya mbali na kupunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya na kupunguza idadi ya vifo vya uzazi kutokana kupata huduma hiyo kupatikana jirani na makazi ya wananchi.

Kata ya Igalla ina wakazi 17,000 kwa mgawanyo wa wanawake 8,043 na wanaume 8,957.

Mbunge wea Ukerwe, Joseph Mkundi aliiomba serikali kuona umuhimu wa kuweka zahanati katika visiwa vidogo vilivyopo wilayani humo ili kuondoa adha ya watu kusafiri muda mrefu kufuata huduma za afya.

# CCM yazifuatilia nyayo za rushwa

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI mpya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dar es Salaam, Abbas Mtemvu amewaonya wala rushwa ndani ya chama hicho, akisisitiza kuwa wakibainika "watakwenda na maji".

Amesema hatakuwa tayari kuona mtu anapitishwa kuwa diwani au mbunge kwa njia ya rushwa na kwamba chini ya uongozi wake, hilo halitotokea.

Mtemvu aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa mwaka wa fedha 2021/22 katika Kata ya Kivukoni. Taarifa hiyo iliandaliwa na Diwani wa Kivukoni, Sharik Choughule.

"Katika nafasi yangu hii mwenyekiti mliyonipa kwa kura nyingi, nisingependa kuona diwani au mbunge anatoa rushwa, sitomvumilia kwa lolote lile, nitamwadabisha kwa mujibu wa kanuni na sheria zilizopo ndani ya chama," alionya.

Mtemvu alisema rushwa inaweza kusababisha wapigakura kupata viongozi wabovu wasioweza kuleta maendeleo kwenye kata au jimbo.

Aliwataka wana CCM wa mkoa wake kuwa na umoja na mshikamano ili kuhakikisha ifikapo mwaka 2025, mkoa wao utoe kura nyingi kwa wagombea wa chama chao na kuendelea kuongoza nchi kwa miaka mitano mingine.

Diwani wa Kivukoni, Choughule, alisema hadi sasa wamefanya mambo mengi ya maendeleo, licha ya kuwa na kikwazo cha kukosa ofisi ya huduma katika kata hiyo.

"Tunakuomba utusaidie ili tuweze kuwa na ofisi ya kata yetu kwani hatujapata eneo la kujenga," alisema Choughule.

Diwani huyo pia alisema amegharamia ununuzi wa boti ya kisasa ya doria kwenye Bahari ya Hindi yenye thamani ya Sh. milioni 55 ambayo inaendelea kufanya kazi.

Mtemvu alipokea ombi la diwani la kutaka ofisi ya kata na kumwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala kulishughulikia upatikanaji wa ofisi ya kata ya Kivukoni ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kwenye Kata ya Kivukoni, Mtendaji wa Kata hiyo, Neema Heddi alisema katika elimu wana shule sita zikiwamo tatu za msingi na nyingine za awali, zilizonufaika katika mpango wa mwaka wa fedha 2022/23 kwa kupatiwa Sh. milioni 90 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya shule.



Kamanda wa Kikosi cha Polisi cha Wanamaji, ACP Moshi Sokoro, akionyesha shehena ya madumu ya mafuta ya kula 3,500 ya lita 20, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuyakamata kisiwa cha Kwale, wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, yakisafirishwa bila kibali kutoka Zanzibar kwenda Lindi. Watuhumiwa 10 wako mbaroni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni wakidaiwa kukutwa na madumu 3,500 ya mafuta

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji limewakamata watuhumiwa 10 wakidaiwa kusafirisha bila kuwa na kibali shehena ya mafuta ya kula madumu 3,500 yenye ujazo wa lita 20 kila moja.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamanda wa Kikosi cha Polisi cha Wanamaji, Moshi Sokoro iliyotolewa jana, madumu hayo yalikamatwa Kisiwa cha Kwale, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani Alhamisi iliyopita majira ya saa 8:30 mchana yakiwa kwenye jahazi lililokuwa likitoka Zanzibar kwenda Lindi.

Alisema Kikosi Kazi cha Polisi Wanamaji Dar es Salaam kilimkamata nahodha wa jahazi hilo, Amme Maulidi (37) mkazi wa Pemba, akiwa na wenzake tisa, kupitia operesheni ya kudhibiti uhalifu ukanda wa Bahari ya Hindi.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa kwenye jahazi kubwa aina ya Bumu lililopewa jina la MV. YESHASEMWA lenye namba za usajili Z.2025 likiwa limebeba mafuta hayo ya kula aina ya Viking.

"Upelelezi wa awali umeonyesha kuwa mzigo huu hauna vibali vya kusafirisha kutoka mamlaka husika Zanzibar, Jeshi la Polisi linashirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na idara nyingine za serikali kuuhakiki na baadaye taratibu nyingine za kisheria zichukuliwe," alisema.

Kamanda Sokoro aliwapongeza wananchi wanaochukia uhalifu ambao wamekuwa wakitoa taarifa ili hatua zichukuliwe.

Alitoa onyo kwa wafanyabiashara wasio waadilifu kwa kuwataka wafuate taratibu za TRA kwa kuwa kinyume chake watakuwa wakikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
25 - 11- 2022

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAPILI** tarehe **27/11/2022** kampuni ya **ICHEETAH LOGTECH TANZANIA LTD** itasafirisha Gari zenye vipimo vikubwa kutoka Dar es Salaam kuelekeaa Kigoma Gari hizo zenye namba za usajili:

   **T507DZD/T907DZE na T148EAF/T630EAJ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**I.T507DZD/T907DZE** Urefu-20m Upana -4.4m ,Kimo-4.8m
**II. T148EAF /T630EAJ** Urefu-20m Upana -4.4m ,Kimo-4.8m

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam** hadi Kigoma Kupitia **Dodoma** gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

17167902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KILOSA**

**S.L.P 29**
**KILOSA**

**19/10/2022**

**YAH: MAOMBI MADOGO NA. 123/2021**

**HALIMA RAMADHANI NYAULINGO ........MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**LAZARO ZEPHANIA MNG'ANYA ...........WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA LAZARO ZEPHANIA MNG'ANYA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kilosa, Tarehe 30/11/2022 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kusikilizwa. Endapo hautaudhuria , Maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.

**Imesainiwa leo Tarehe 18 mwezi 10 Mwaka 2022**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI N NYUMBA (W)
KILOSA

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARY JACKSON MALEKO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S0266/0027** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **REGINAMUNDI GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka **2005.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/454924/2022**

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 25/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU GEORGE JOHN JAKA WA KIGURUNYEMBE KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MWANNE RAMADHANI**

**TANGAZO**

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29/ Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 15 mwezi 11 mwaka 2022**



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma, Dk. Hamisi Mkanacha (kushoto), akikabidhi hati miliki ya kimila kwa mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Haubi, ambayo imetolewa na Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais chini ya Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame nchini (LDSF), wilayani humo, juzi. **PICHA: OMR**

# Spika aonya utendaji UVCCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson amesema vijana wa Umoja wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) wanapaswa kueleza mazuri yaliyofanywa na viongozi wakuu wa nchi na kuwalinda kwa hoja badala ya kusubiri watu wanaoanzisha vioja ili wawajibu.

Kiongozi huyo alitoa angalizo hilo jana alipozungumza jana jijini hapa kwenye bonanza la vijana wa Green Marathon lililoandaliwa na UVCCM kuelekea uchaguzi mkuu wa umoja huo taifa uliopangwa kufanyika leo jijini.

Alisema wajibu wa vijana ni kuwalinda viongozi wao, akisisitiza kuwa ndilo jukumu la msingi kwao wanalopaswa kulitambua kila wakati.

"Kuja hapa iwe ni chachu ya hamasa na mnaporejea endelezeni mazoezi kwa kueleza kazi nzuri inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, msikae kimya, waelezeni wananchi.

"Kiongozi anapaswa kulindwa kwa hoja, eleza mambo ambayo viongozi wetu wakuu wa nchi hii wanayafanya katika maeneo yenu, ngazi ya wilaya eleza na ya taifa.

"Lakini kwenye wilaya yako yapo na umenyamaza husemi, kazi yako kijana kumlinda kiongozi wako kwa hoja, inawezekana inajengwa barabara lakini SGR haijafika, wewe unafika pale unawaeleza SGR hawaijui na hawajaiona wewe waeleze mradi uliopo pale," alisema. Spika Tulia alisema wasisubiri watu waanzishe vioja ndipo waanze kazi ya kuwajibu. "Anzisha wewe hoja, wakibisha wape na data, sisi siyo watu wa kuanzishiwa vioja ndipo tuanze kubisha, sisi ni watu wa kuanzisha hoja, walete vioja tuwarudishie hoja," alisema.

Dk. Tulia ambaye kitaaluma ni mwanasheria, aliwataka kujiepusha na vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya ili kulinda afya zao.

Kuhusu uchaguzi, aliwataka kuchagua viongozi watakaofanikisha kukipigania chama katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

"Mama anataka kesho (leo) mkamilishe jambo lake kwa kumchagulia viongozi, wale wote waliorejeshwa kugombea wanafaa ila wanatakiwa wapatikane wachache miongoni mwao, ndiyo demokrasia, wengi wakisema huyu tutakwenda naye hadi kwa Samia," alisema.

Alisema moto uliowashwa kwenye mikoa na wilaya usizimwe bali uendelee, hivyo wahakikishe wanaimarisha chama na jumuiya.

Katibu Mkuu wa UVCCM, Kenani Kihongosi alisema vijana wanapaswa kutambua wagombea waliopitishwa, wote wana fursa ya kuchaguliwa.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Leyla Ngozi alimpongeza Kihongosi kwa kazi anayofanya na watendaji wake kwa kuimarisha umoja huo.

# Serikali yakabidhi hati za kimila 300

**Na Mwandishi Wetu,** KONDOA

SERIKALI imekabidhi hati miliki za kimila 305 kwa wananchi wa vijiji vya Haubi na Mafai wilayani Kondoa mkoani Dodoma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame nchini (LDSF).

Akikabidhi hati hizo jana, Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Dk. Hamisi Mkanacha aliishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais inayotekeleza mradi huo kwa ushirikiano na Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi kwa kufanikisha utolewaji wa hati hizo.

Alisema kupatikana kwa hati hizo ni fursa kubwa kwa wananchi wa vijiji hivyo na wilaya kwa ujumla kwa kuwa zitawasaidia kuepusha migogoro ya ardhi na kuwawezesha kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha. Hata hivyo, Dk. Mkanacha aliwataka wanufaika wa mradi huo kuheshimu matumizi ya ardhi yaliyopangwa na kuwa ni kosa kisheria kuitumia kwa namna nyingine.

Aliwataka viongozi wa ngazi mbalimbali wilayani humo kusimamia kikamilifu mipango ya ardhi iliyowekwa ili wananchi wasiende kinyume, hali inayoweza kuibua migogoro.

"Ndugu zangu wananchi, baadhi ya maeneo utakuta mnapanga matumzi ya ardhi lakini anatokea mtu mmoja mjuaji, mjanja anatafuta mteja anamuumizia ardhi. Kwa hili tutakuwa wakali mno," alionya.

Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa LDFS, Joseph Kihaule alisema hati miliki za kimila zinazotolewa hazihamishiki na zinabaki kwa ndugu husika, hivyo hairuhusiwi kuuzwa.

Pia alisema mojawapo ya faida za hati hizo ni kuwa hazitalipiwa kodi ya mwaka kama ilivyo kwa hati zingine za mijini, hivyo wananchi wana fursa ya kutumia ardhi hiyo kwa maendeleo endelevu.

Akizungumzia shughuli zingine za mradi huo, Kihaule alisema kwa sasa vijiji vya Haubi na Mafai vinatarajia kuchimbiwa visima ili kupunguza makali ya ukame unaokabili wilaya hiyo.

Shughuli zingine kupitia mradi huo ni kuundwa kwa vikundi vya uzalishaji mali ikiwamo ufugaji wa nyuki, mifugo pamoja na uchimbaji wa visima ambavyo vikikamilika vitatumika katika umwagiliaji.

# India yaombwa kuwasaidia walio nje mfumo wa elimu

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dk. Michael Ng'umbi ameiomba India isaidie vijana wa kitanzania walio nje ya mfumo wa elimu, kupata mafunzo ya nishati jadidifu ambayo watayatumia kubuni vitu vya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Ng'umbi aliwasilisha ombi hilo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya siku ya ushirikiano wa kiufundi na kiuchumi kati ya Tanzania na India (ITEC) yaliyoandaliwa na Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Ng'umbi alisema India imekuwa na programu ya kusaidia watanzania kupata ufadhili na kusoma nchini mwake, hivyo kuongeza nguvu kazi inayosaidia kuijenga nchi.

"Tunahitaji vijana wenye elimu na ujuzi hasa kwenye eneo la teknolojia na wenzetu India wapo vizuri kwenye hili na pia kwenye teknolojia ya viwanda vidogo. Balozi amezungumzia programu ambazo wanazo, nafasi ambazo zipo, ametueleza nafasi zipo nyingi na watanzania wanatakiwa kuzichangamkia.

"Hili ndilo ambalo ningependa watanzania wengi wafahamu kuwa kupitia mpango wa ITEC, tumeelezwa kuwa ni theluthi moja ya hizo nafasi ambazo zimeshachukuliwa, tuna theluthi mbili ya nafasi ambazo bado watanzania tunapaswa kuzichangamkia kwenda kusoma," alisema.

Kiongozi huyo alisema vijana ambao wapo nje ya mfumo wa elimu siyo kwamba ni wajinga au hawana maarifa, bali wamejikuta huko kwa sababu hawajapata fursa ya elimu.

"Wakipewa fursa ya elimu watafanya makubwa, ombi langu kwa Ubalozi wa India kama mnaweza kusaidia, bado kuna watanzania wengi ambao hawapo shuleni.

"Taasisi yetu inashughulika na vijana hawa ambao wapo nje ya shule, tupo tayari kufanya kazi na India ili tuwafikie watanzania wengi zaidi ambao wapo nje ya shule na waliopo shuleni," alisema,

Pia alisema janga la UVIKO-19 limewafundisha kwamba watu wanaweza kusoma bila kusafiri kwenda nchi nyingine.

"Duniani kote wameshajua kwamba kumbe inawezekana kufundisha watu huko waliko na gharama ikapungua, wito wangu tunaweza kuchangamkia fursa, siyo lazima uende kule, unaweza kusoma kupitia teknolojia mtandao," alisema. Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan alisema nchi yao ni mshirika mkubwa wa Tanzania na kupitia ITEC kila mwaka hutoa nafasi 450, akibainisha zilizobaki ambazo alitaka watanzania wazichangamkie ni 150.

Alisema ITEC imekuwa ikitoa mafunzo ya aina tofauti yakiwamo ya uandishi wa habari, kilimo na teknolojia ambayo yana tija kwa taifa. Balozi Pradhan alisema hadi sasa wanafunzi 100 wa Tanzania wamepelekwa India kwa ajili ya mafunzo ya kuwajengea uwezo na baadhi yao tayari wameshamaliza.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo, Msimamizi wa Miradi ya Nishati Jadidifu kutoka Shirika la Maendeleo (NDC), Fanikio Mwaipula alisema alipata mafunzo ya nishati jadidifu yaliyotolewa kwa mwezi mmoja.

"Nilichojifunza wenzetu wamewekeza katika nishati jadidifu na wana miradi mikubwa, Tanzania tunaweza kuiga kwa sababu nishati hii tunaona inatumika vijijini tu lakini tunaona serikali imeanza kuifanyia kazi, nishati hii inapatikana kipindi chote," alisema.

# Rais: Burundi imeipokea benki ya CRDB

**BUJUMBURA,** BURUNDI

RAIS wa Jamhuri ya Burundi, Evariste Ndayishimiye ameipongeza Benki ya CRDB Burundi kwa mafanikio makubwa iliyopata katika kipindi cha miaka 10 ya kuwapo kwake Burundi na kusema kuwa nchi hiyo imeipokea benki hiyo kwa mikono miwili na inajivunia kuwapo kwake nchini humo.

Rais Ndayishimiye alitoa pongezi hizo katika mkutano na ujumbe wa Benki ya CRDB ulioongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela aliyefuatana na na Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi ya Kampuni Mama ya Benki ya CRDB pamoja na kampuni tanzu ya Benki ya CRDB Burundi.

Ujumbe huo umetembelea Rais Ndayishimiye ikiwa ni mfululizo wa ziara zilizofanywa na viongozi waandamizi wa Benki ya CRDB na kutoa shukrani wa serikali na wadau mbalimbali ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika miaka 10 ya utoaji huduma za Benki ya CRDB Burundi.

Akizungumza katika mkutano huo, Rais wa Jamhuri ya Burundi, Evariste Ndayishimiye alisema Tanzania na Burundi ni ndugu wa karibu na hata mipaka iliyopo ni matokeo ya historia ya ukoloni lakini mipaka hiyo kamwe haiwezi kuwa kikwazo cha uhusiano mzuri kati ya nchi hizo mbili zenye historia kubwa ya ushirikiano.

"Tunashukuru kuwa Tanzania ilishiriki kwa kiasi kikubwa sana katika kupatikana kwa amani nchini Burundi na sasa mnakuja tufanye maendeleo kwa pamoja kwa manufaa ya nchi zetu lakini pia Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki," alisema Rais Ndayishimiye ambaye katika mkutano wa 22 wa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Julai 2022 alitangazwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Rais Ndayishimiye aliingia maradarakani mnamo mwezi Juni 2020 ambapo katika kipindi chake Benki ya CRDB imeendelea kufanya vyema sokoni hadi kufikia kushika nafasi ya tatu kati ya benki 13 zinazotoa huduma za kibenki nchini Burundi.

Katika kipindi hicho, benki hiyo imeweza kufungua matawi manne huku tawi la tano likitarajiwa kufunguliwa mapema mwakani katika makao makuu ya mapya ya nchi ya Burundi, Gitega.

"Tunawashuru sana kwa jitihada zenu ya kutoa elimu ya fedha kwa Warundi ili wajifunze namna nzuri ya usimamizi wa fedha na kuweka lakini pia tungependa kushirikiana nanyi zaidi katika programu za vijana na wanawake ambao ni kipaumbele chetu kikubwa kwa sasa," aliongeza Rais Ndayishimiye.

Pia alituma salamu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akisisitiza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ni dada yake ambaye wanashirikiana vyema katika uongozi wao. Rais Ndayishimiye alitoa wito kwa Benki ya CRDB Burundi kukaa pamoja na idara maalum inayoshughulika na mipango mikakati ya Serikali ya Burundi ili kuangalia maeneo ya kushirikiana zaidi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela aliishukuru Serikali ya Burundi kwa ushirikiano mkubwa kwa Benki ya CRDB Burundi uliopelekea kampuni tanzu hiyo kupata mafanikio makubwa ndani ya kipindi kifupi cha miaka 10.

Sambamba na hilo, Nsekela aliishukuru Serikali ya Rais Ndayishimiye kwa kuipatia eneo Benki ya CRDB Burundi katika makao makuu mapya ya nchi, Gitega ili kufanikisha ujenzi wa tawi jipya.

"Nilipata bahati ya kushiriki katika mikutano yako pamoja na Rais Samia na niliona kiu yenu ya kuona ushirikiano wa sekta binafsi za Tanzania na Burundi, hivyo nikuahidi kuwa Benki ya CRDB itaendelea kuunga mkono jitihada zako za kukuza uchumi wa Burundi kwa manufaa ya watu wa Burundi lakini pia Tanzania na Jumuiya nzima ya Afrika Mashariki," alisema Nsekela.

Aliongeza kuwa Benki ya CRDB inatarajia kuingia DRC hivi karibuni ambapo inatarajia kufungua matawi katika mikoa iliyo karibu na mpaka wa Burundi na DRC ili kuchochea biashara kati ya nchi hizo mbili ambazo ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Tutajikita katika matumizi ya teknolojia ili kuweza kujumuisha Warundi wengi zaidi katika mfumo rasmi wa kifedha ambapo ninafurahi kuwa mpango wetu wa kutumia wakala umeendelea kufanya vyema ambapo hadi hivi sasa tuna mawakala zaidi ya 600 wanaosaidia kutoa huduma kwa matawi yaliyopo," alisema Nsekela.

Alibainisha kuwa uwezo wa Benki ya CRDB sambamba na washirika wake wa kibiashara unaipa nguvu kubwa benki katika kuwezesha sekta mbalimbali ambapo hivi karibuni benki imeingia makubaliano na mashirika makubwa ya fedha kama IFC, PROPARCO na INTESA ambapo dola milioni tano za Marekani zimeelekezwa katika kuwezesha biashara ndogo na kati Burundi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni Mama ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay alitoa shukrani kwa Rais Ndayishimiye na serikali yake kwa ushirikiano uliochangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya Benki ya CRDB Burundi katika kipindi cha miaka 10 tangu kuingia katika soko la Burundi.

"Wakati tunafanya uamuzi wa kufungua biashara yetu nchini Burundi haikuwa rahisi kufikia uamuzi ule kwa kuwa ilikuwa ni mara ya kwanza tunafungua biashara nje ya nchi na maswali yalikuwa mengi juu ya uamuzi wa kuchagua Burundi lakini leo hii sote tunajivunia na kuona nchi zote mbili zinanufaika ambapo hapa Burundi tunalipa kodi na kutoa ajira lakini pia faida inayopatikana hapa inawanufaisha wanahisa wetu hadi Tanzania," alisema Dkt. Laay.

Mwenyekiti wa Benki ya CRDB Burundi, Hosea Kashimba alitoa shukrani zake kwa Rais Ndayishimiye na kusema kuwa mapinduzi makubwa ya uchumi yanaonekana nchini Burundi katika kipindi chake na moja ya sekta ambayo inafanya vizuri ni sekta ya ujenzi, jambo linaloashiria imani kubwa ya wawekezaji kwa serikali.

# Wanaume waitwa upimaji wa VVU

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga amewataka wanaume kujenga tabia ya kwenda vituo vya kutolea huduma ili kupima afya zao ikiwamo kuangalia kama wana maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) au la.

Ndemanga alitoa rai hiyo jana wakati akifungua Maadhimisho ya Wiki ya Ukimwi Duniani, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Zainab Telak.

Akizungumzia maadhimisho hayo ambayo kitaifa yanafanyika mkoani Lindi, kiongozi huyo alieleza kushangazwa na baadhi ya wanaume ambao wamekuwa wazito kujitokeza kupima afya zao ili kujua kama wapo salama au la.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2016/17, wanawake waliojitokeza kupima walikuwa asilimia 55.9 ya waliojitokeza kupima.

"Hali hii ni hatari sio tu kwa mtu binafsi au kaya, bali pia kwa taifa kwani hudhoofisha jitihada za serikali na wadau katika mapambano ya kutokomeza VVU. Ninaomba wananchi mtumie maadhimisho haya kujitokeza kupima na huduma zinatolewa bila malipo.

"Wanaume wenzangu tunakwama wapi? Kila jambo tunazidiwa, kupima afya tunazidiwa, idadi (kwenye sensa ya watu na makazi) tunazidiwa ni wakati wa kujitafakari sasa," alisema.

Ndemanga alisema baadhi ya wanaume wamekuwa wakitafsiri majibu ya VVU kutoka kwa wenza wao wanaokwenda vituo vya kutolea huduma kupima afya zao, kwamba wanapokutwa hawana maambukizi na wao hujiona wapo salama, kitu ambacho siyo sahihi.

Alisema kitendo cha wanaume kutumia matokeo ya wenza wao ni kujidanganya na kuwataka wajitokeze kupima ili kufahamu usalama wa afya zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko aliitaja kaulimbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni 'Imarisha Usawa' ambayo inalenga kuyaangalia makundi ya watu wote walioachwa nyuma katika elimu ya upimaji VVU likiwamo kundi la wanaume linalotajwa kuwa ni wazito kujitokeza kupima afya.

Dk. Maboko alisema bado wanaume wanaongoza kwa vifo vitonavyo na Ukimwi ilhali wanawake ndiyo wanaoongoza kwa kupata maambukizo mapya.



Kondakta wa daladala lenye namba za usajili T 124 DQL, linalofanya safari zake kati ya Tegeta Nyuki na Mbezi Mwisho kupitia Madale, mkoani Dar es Salaam, akiwa amevaa sare za kazi huku suruali ikining'inia kwenye mapaja, jana. Makondakta pamoja na madereva ni kama vile hawataki kuvaa sare hizo wakati wengine wakishangaza kwa uchafu, uchakavu na kupauka kwa nguo hizo. **PICHA: JOHN BADI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Jamii inapaswa kuwajibika ulinzi wa vyanzo vya maji na utunzaji wa mazingira*

**MABADILIKO** ya tabianchi yamezidi kuikumba dunia na kusababisha athari kubwa kwa binadamu na viumbe hai vingine ikiwamo wanyama na mimea. Sababu kubwa ya tatizo hilo ni shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji usiozingatia kanuni za uhifadhi na utunzaji mazingira.

Sambamba na sababu hizo, mabadiliko ya tabianchi yamesababishwa na ukataji ovyo wa miti na misitu kwa ajili ya ujenzi na nishati ya kupikia kwa maana ya kuni na mkaa, kilimo na ufugaji katika vyanzo vya maji.

Kutokana na shughuli hizo za kibinadamu, hivi sasa kumekuwa na vilio kila kona ya nchi kuhusu kukosekana kwa umeme, maji na chakula kulikosababishwa na ukame. Pia tumeshuhudia mifugo ikifa kwa kukosa maji na malisho vilivyosababishwa na ukame ambao chanzo kikuu ni mabadiliko ya tabianchi.

Takribani mwezi sasa, wananchi katika maeneo mbalimbali wamekuwa wakilalamikia mgawo mkali wa umeme ambao sababu kubwa ni kupungua kwa maji katika mabwawa ya kuzalisha nishati hiyo.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wiki hii lilikiri kuwa hali ya upatikanaji wa umeme ni mbaya huku likiweka bayana kuwa kuna upungufu wa megawati 350 uliotokana na ukosefu wa mvua za kutosha uliosababishwa na ukame ambao kwa kiasi kikubwa chanzo ni mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, wakati wa mgawo mkali wa maji katika mikoa ya Dar es Salaam, Rais Samia Suluhu Hassan alisema shughuli za kibinadamu zikiwamo kilimo na ufugaji kwenye mito pamoja na uharibifu wa vyanzo vya maji, vimesababisha taabu kwa maisha ya binadamu ikiwamo ukosefu wa maji na umeme.

Bila kuuma maneno, Rais Samia alisema katika Mto Ruvu kuna zaidi ya ng'ombe 5,000 ambao licha ya kuharibu mazingira pia ni chanzo cha kupungua kwa maji kutokana na kunywa mamilioni ya lita. Pia alisema kumekuwa na uharibifu mkubwa wa chanzo cha Mto Ruvu katika milima ya Uluguru kwa sababu ya uchomaji misitu.

Timu ya waandishi wa habari wa Nipashe ilisambaa maeneo mbalimbali ripoti maalum zilizoibua matatizo katika jamii yaliyosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi yakiwamo vifo vya mifugo, mito kupungua maji na mingine kukauka na baadhi ya mabwawa kuwa katika hatari ya kukauka.


Ripoti hizo pia ziliibua adha wanazopata wananchi hususan wanawake kutembea umbali mrefu kutafuta maji huku wakiweka rehani ndoa zao pamoja na kutishiwa na hatari ya wanyama wakali.

Mambo yote hayo yanaonyesha dhahiri kwamba kuna hatari kubwa inayowanyemelea binadamu ikiwamo ukosefu wa huduma muhimu kama maji, umeme na chakula iwapo nguvu ya ziada katika kukabili mabadiliko ya tabianchi hazitachukuliwa.

Kama alivyosema Rais Samia akiwa katika moja ya ziara zake hivi karibuni mikoani kwamba majanga yanayoikumba nchi ni kutokana na maovu tuliyoyatenda, hivyo tunahukumiwa kwayo, ni wajibu wa jamii kubadilika na kutunza mazingira na kulinda vyanzo vya maji.

Badala ya kuendelea kuharibu vyanzo vya maji na mazingira, kila Mtanzania awe askari namba moja katika ulinzi na kuhifadhi mazingira kwa ustawi wa taifa na watu wake. Kwa kufanya hivyo, hali ya mazingira itarejea katika hali yake kwa Tanzania na Dunia kwa ujumla kuwa sehemu salama kwa kuishi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mtindo wa sheria mkononi unaumiza, tuachane nao

**KUJICHUKULIA** sheria mkononi, ni kitendo cha kumwadhibu mtu ambaye amefanya kosa bila kuifuata sheria, kanuni na taratibu za nchi, kinatajwa ni kosa la jinai na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Sababu ya kuitwa jinai na ukiukwaji wa haki za binadamu, ni kwamba mtu au watu wanapojichukulia sheria mkononi, wanazuia nafasi ya vyombo vyenye mamlaka kama polisi kutimiza majukumu yao.

Pamoja na serikali kuzuia wananchi kujichukulia sheria mkononi kitendo ambacho husababisha baadhi ya watuhumiwa kupoteza maisha, bado baadhi yao wanaendelea na mtindo huo unaoumiza hata wasio na hatia.

Katika mazingira hayo, wapo baadhi ya watu wanaouawa kwa tuhuma za wizi, ushirikina na mambo mengine yanayoendana na hayo, huku wakiwa hawana hatia na hivyo kujikuta wakipoteza maisha.

Lakini hata kama watakuwa wana hatia ya wizi au ushirikina, ninaamini hakuna binadamu mwenye haki ya kutoa uhai wa mwenzake, na ndio maana vyombo vya dola huwa vinahimiza umuhimu wa kufuata sheria.

Vinaposema kufuata sheria, maana yake ni kama mtu anatuhumiwa kwa jambo lolote akamatwe na kufikishwa katika kituo cha polisi au kwa viongozi wa serikali kwenye eneo alilopo, kwa ajili hatua zaidi za kisheria.

Lakini ajabu ni kwamba, badala ya kuzingatia maelekezo hayo, baadhi ya watu wanapotuhumu wengine kwa wizi au jambo lolote, huamua kujichukulia sheria mkononi kwa kumpiga mawe au kuwachoma moto hadi kufa.

Mfano mmojawapo wa kujichukulia sheria mkononi ni mauaji ya aliyekuwa Mwalimu wa Shule ya Msingi Livingstone, Erick Mbilinyi, mkazi wa mtaa wa Mgendela, Halmashauri ya Mji wa Njombe anayedaiwa kuuawa na wananchi wenye hasira kali wakimtuhumu kuwa ni mwizi.

Inaelezwa kuwa tukio hilo lilitokea Novemba 20, mwaka huu majira ya saa 10:00 jioni katika eneo la Shule ya Msingi Selestini, mtaa wa Joshoni, baada ya wananchi hao kumwita mwizi.

Alituhumiwa kuingia katika moja ya nyumba mjini hapo, ndipo wananchi wakajichukulia sheria mkononi kwa kimpiga hadi kumuua bila kujiridhisha zaidi, kwa kuwa inaelezwa na wenzake kuwa hakuwa na tabia za wizi.

Baadhi ya walimu wenzake waliwaambia waombolezaji kuwa mwenzao alikuwa na tatizo la akili hali ambayo ilikuwa ikimtokea mara kwa mara na kusababisha afanye mambo ambayo mwisho wake yamepoteza uhai wake.

Ninadhani kwamba ipo haja sasa kwa wananchi kutambua kuwa hakuna mwenye haki ya kutoa uhai wa mwenzake, lakini pia kuachana na haraka ya kuchukua hatua kama hizo bila kujipa nafasi kumhoji mtuhumiwa.

Vilevile ni vyema kuachana na mtindo wa 'kuimbiwa wimbo wa mwizi' na kuchukua sheria mkononi bila hata kujipa muda wa kuhoji huo wizi umetokeaje na katika mazingira gani.

Ikumbukwe kuwa wapo baadhi ya walevi ambao hukosana na wenzao na kuwavizia katika maeneo ambayo wanaamini wanaweza kuwadhuru kwa kupiga kelele za mwizi, ili makundi ya watu yajitokeze na kuwaumiza.

Matukio ya kujichukulia sheria mkononi yanagusa hata kwenye familia, kwani taarifa ya matukio ya ukatili iliyotolewa na Jeshi la Polisi kwa waandishi wa habari mwaka jana, inaibua matukio 908 ya wanandoa kuuana na kujiua.

Kwa mujibu wa Msemaji wa jeshi hilo, SACP David Misime, kuanzia mwaka 2019 hadi Septemba 30 mwaka jana, wanaume 750 wameua wake zao, huku 74 kati yao wakiwa wamejiua wenyewe baada ya kuua.

Wanawake 158 nao wameua waume zao, 39 kati yao wakiwa wamejiua wenyewe baada ya kumaliza kuua wenza wao, huku mchanganuo wa SACP Misime ukionyesha kuwa wanaume walioua wake zao mwaka 2019 walikuwa ni 328, huku waliojiua baada ya kuua wake zao wakiwa ni 28.

Nao wanawake walioua waume zao walikuwa ni 58, huku 18 kati yao wakiwa wamejiua baada ya kufanikisha mauaji hayo. Kwa mwaka 2020, anataja idadi ya wanaume walioua wake zao kuwa ni 226, lakini 30 kati yao wakiwa wamejiua baada ya kuua wake zao.

Idadi ya wanawake walioua waume zao anaitaja kuwa ni 71, huku 12 kati yao wakijiua baada ya kuua waume zao, na kwamba kufikia Septemba 30 mwaka jana, wanaume walioua wake zao walikuwa ni 156, waliojua baada ya kuua wakiwa ni 16, na wanawake walioua waume zao ni 29, huku tisa kati yao wakijiua baada ya kufanya vitendo hivyo vya kujichukulia sheria mkononi.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Ibara ya 18 iheshimiwe! kusifu ni haki, kukosoa ni haki, sio chuki



Pascal Mayalla

KWA maslahi ya taifa. Makala ya leo ni kuhusu moja ya haki muhimu sana ndani ya katiba, yetu ya JMT ya mwaka 1977, kuanzia Ibara ya 18 - 24, katiba yetu imetoa haki zifuatazo: 18 ni uhuru wa maoni, 19 uhuru wa mtu kuamini dini atakayo, 20 ni uhuru wa mtu kushirikiana na wengine, 21 ni uhuru wa kushiriki shughuli za umma, 22 ni haki ya kufanya kazi, 23 ni haki ya kupata ujira wa haki na 24 ni haki ya kumiliki mali.

Haki hizi sio hisani kusema zinaweza kutolewa au laa! Haki hizi ni stahili, zinapaswa kutolewa na kuheshimiwa na Watanzania wote ikiwamo serikali na viongozi na taasisi zote. Kwa leo nitajikita zaidi kwenye Ibara ya 18, inasema:

"(1) Bila ya kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, na kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi, na pia ana uhuru wa kutoingiliwa katika mawasiliano yake.

"(2) Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii."

Haki hizi na uhuru huu wa kutoa maoni unaokwenda sambamba na mipaka ya kawaida ya uhuru, yaani hakuna uhuru usio na mipaka, mwisho wa uhuru wako ni pale uhuru wa mtu mwingine unapoishia.

Huu uhuru wa kutoa mawazo yako, unapaswa kuheshimiwa na wote, hata kama hukubaliani na mawazo hayo, na wewe pia unapaswa kuheshimu uhuru, maoni na mawazo ya wengine, hata kama hukubaliani nayo.

Leo nimejikita kwenye ibara hii, kufuatia juzi kati hapa, kuna mtu ametoa mawazo yake kuhusu jambo fulani, mtu huyo ameshambuliwa kila kona kwa kushukiwa kama mwewe anavyotaka kunyakua kifaranga cha kuku, wengine wakimbeza, wengine wakimdhihaki na wengine hata kufikia kiwango cha kumtukana na kumdhalilisha!

Kilichopelekea mtu huyo kushambuliwa, ni kwa sababu tu amekosoa jambo fulani!. Kutokana na kutoa nawazo yake ya ukosoaji, ninaona kuna watu wanataka kuingilia haki hii muhimu na kujimilikisha wao kwa kuingilia uhuru wa maoni wa watu wengine na hata kuwapangia ni maoni gani watoe! Yaani wenye haki ni wanaosifu tu na kupongeza, lakini ukikosoa, inakuwa nongwa.

Toka enzi za Rais Mwinyi, Rais Mkapa, Rais Kikwete na Rais Magufuli, wote walisifiwa na walikosolewa! Ile haki ya kusifu na kupongeza, inapaswa kwenda sambamba na haki ya kukosoa!

Hivyo, kuna watu wanataka haki iwe na haki ya kusifu tu na kupongeza tu, lakini kukosolewa iwe nongwa, ni kosa, ni dhambi!

Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia katika mkutano wa 47 wa wanasheria Afrika Mashariki uliofanyika mkoani Arusha, amesema haya kuhusu kushirikisha watu/taasisi ambazo ziko dhidi yake.

"Kwa mfano Tanzania, miaka minne mitano iliyopita tulikuwa na Tanganyika Law Society ambayo frankly speaking ilikuwa siyo chama cha wanasheria, kilikuwa chama cha wanaharakati na mapambano yao yalikuwa ni dhidi ya serikali.

"Sasa mimi nikijua wewe ni dhidi yangu nitakushirikishaje? Siwezi kukushirikisha, si ndiyo! Mpaka unionyeshe kwamba am here to support you, I'm here to serve a country, I'm here kuonyesha ujuzi wangu kwa nchi yangu.

"Nikikuona una sura hiyo nitakushirikisha, nikikuona una sura ya uadui nami sitaweza kukushirikisha. Utatumia sheria zote za kimataifa, zoooote na mimi nitatumia zangu za ndani ya nchi usishiriki kwangu."

Kukosoa serikali, sio kuwa dhidi ya serikali, wala ukosoaji, sio uadui, sio chuki, na sio dhidi ya serikali, amlimradi ukosoaji huo uwe ni ukosoaji wenye nia njema ya kuisaidia nchi, kuisaidia serikali na kuwasaidia viongozi, ambao unaitwa constructive cricism, ukosoaji wenye nia ya kujenga na kusaidia, ambao huendana na ushauri wa njia bora ya kufanya hilo jambo unalokosoa.

Kwenye Freedom of expression ni haki kwa wote, wenye kusifu na kupongeza, wana haki ya kusifu na kumpongeza kwa kuupiga mwingi, na wenye kukosoa wana haki ya kukosoa, hivyo haki ya kusifu inakwenda sambamba na haki ya kukosoa, ibara ya 18 ya katiba inataka haki ya kusifu iheshimiwe na haki ya kukosoa iheshimiwe.

Hivyo kama ilivyo kwenye haki ya kupiga kura, inakwenda sambamba na haki ya kupigiwa kura, vivyo hivyo kwenye haki ya kusifu na kupongeza viongozi, haki hiyo ya kupongeza, inakwenda sambamba na haki ya kukosoa viongozi, mkosoaji asishambuliwe yeye, ishambuliwe hoja yake!

Wanaosifu wasifu kwa hoja, ni haki yao kusifu, lakini pia wanaokosoa, wakosoe kwa hoja kwa kutumia ukosoaji wa wenye nia njema ya kujenga, kwa kutumia lugha ya staha.

**Wasalaam**
**Paskali Mayalla**
**+255 754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Watanzania tunatia fora kwa kujisahau



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HISTORIA ya kidini inatwambia kuwa Mungu kwanza kabisa aliumba mbingu na nchi, katika nchi akaweka mimea, maji, wadudu, ardhi na wanyama. Kisha akatuumba sisi watu, kabla ya binadamu.

Sisi watu akatwambia enendeni mkaitawale dunia, kwa maana kwamba na kila kitu kilichomo. Inaonekana tuliumbiwa mbinguni na ndiyo sababu akatwambia enendeni mkavitawale, ni alipotushusha.

Ndiyo maana hata tunapofariki dunia, huambiwa kuwa tunakwenda mbinguni na huko tunagawanyika wenye dhambi na wasio na dhambi, kila mmoja akienda anakostahili, kwa matendo yake duniani.

Tuliendelea kuitwa watu hadi hapo historia nyingine ya kibaiolojia, alipotwambia kuwa aliumbwa Adam na kisha Hawa kutokana na ubavu, hapo tulipozaliwa na wawili hawa baada ya kufakamia tunda walilokatazwa ndipo tukazaliwa sisi kina bin Adam. Ukijua mfumo dume ulianza zamani, hushangai wanawake kuitwa binadamu badala ya binti Adamu.

Tulipambana sana kuitawala dunia, kwani tulifanikiwa kutawala mimea, wadudu na maji, lakini kwa wanyama ilikuwa mbinde kwa sababu tulianza kuwindana, sisi tukiwatafuta kupata nyama na wao wakitusaka kupata nyama vivyo hivyo.

Baadhi tukawashinda ujanja na kuwatawala tukawafuga, ndio hao sasa unawaona majumbani tukitaka kuwala tunawakamata na kuwachinja, bila kipingamizi na wao bila kutambua kuwa tukishasikia njaa au tukiwa na sherehe shabaha ya kwanza ni kwao.

Lakini huko nyuma, niliwahi kuandika mahali kuwa siku zinakwenda ipo siku wanyama watacharuka na kudai haki zao, na ndipo tutajikuta hatuna pa kwenda bali kubadilishana makazi. Pengine ndiyo sababu kuna fikra kuwa tukishakufa tunarudi duniani katika sura za wanyama.

Angalia sasa katika baadhi ya maeneo nchini, wanyama wanavamia makazi ya watu kusaka maji.

Ni baada ya kuchoka kuona binadamu kila kitu wanakitaka wao huku nao waliumbwa kupata maji hayo hayo, hivyo wakiona wanakufa njaa wanazama majumbani kunyang'anyana maji na binadamu.

Haikuwa nia yangu kuyasema haya leo, lakini muktadha unanilazimisha kufanya hivi kuona jinsi Watanzania tunavyoenenda na maisha yetu kila siku, kana kwamba ama kuna kitu tumesahau au tunajisahaulisha tu, kama si kukosea mahali.

Hivi Tanzania tangu tupate Uhuru, kweli tunaweza kuwa katika hali hii leo ya kujadiliana maji na umeme kila siku mpaka kufikia hatua ya kugawana, mambo ambayo yako ndani ya uwezo wetu? Tangu enzi na enzi tunachagua viongozi ambao lugha yao ni ya kumaliza matatizo ya nchi.

Nenda bungeni kasikilize yanayojadiliwa humo na maswali yanayoulizwa na kujibiwa, utadhani matatizo ndo yamehitimu, lakini wapi. Ndiyo kwanza mambo yanakwenda segemnege! Tatizo liko wapi lakini?

Mtu anayesikia au kuona Tanzania imezungukwa na maziwa makuu katika Afrika, halafu akaambiwa hawana maji na yanayopatikana yanatoka kwa mgawo! Mtu aambiwe eti pamoja na maji yalipo na gesi iliyopatikana, eti hakuna umeme wa uhakika, ataelewa nini?

Siku hizi tena utasikia wataalamu wa Tanzania eti wamekwenda Rwanda kujifunza sijui nini? Wakitoka huko utawasikia wanasifia Rwanda inaunda magari na kutengeneza simu za mkononi, Rwanda ni safi usiombe, lahaula!

Hivi hatukuwa na kiwanda cha magari cha Nyumbu mkoani Pwani kweli au ni ndoto? Kiwanda kilikwenda wapi? Yale magari yalitokomelea wapi Maulana wetu? Huko nyuma tukikata mti tukipanda mti, sasa tunaanza kukatazana kupika kwa kuni na mkaa! Eti vinatuua 33,000 kila mwaka! Tungesalia?

Unaweza kukaa chini ya mti ukajishika kichwa na kuanza kujiuliza hivi bajeti zilizokuwa zinapangwa kuanzia miaka ya sitini mpaka leo, fedha zilikuwa zinaishia wapi wakati matatizo ya wananchi hayamaliziki? Leo bado tunasikika tukiomba misaada na kupewa mikopo tukililia riba nafuu!

Unasikia Balozi anatangaza kwa kujigamba kuwa nchi fulani imeipa Tanzania fedha za kununulia chakula! Jamani tunakwama wapi watu wa Nyerere? Tunaletewa fedha ya kununulia chakula huku tukiwaambia masikini wakulima wetu limeni, vuneni, uzeni kokote ni jasho lenu. Kweli?

Tatizo kuu la Watanzania ni kupata tatizo na kulitatua kwa muda, likinyamaza tunajisahau na kutanua, likirudi hatujajipanga tunaanza kuhaha. Hivi mgawo wa umeme na maji ni vya leo?

Huko nyuma hamkumbuki hata Dk. Magufuli kabla hajaaga, alizungumzia sana majenereta ya Kariakoo yanayolia tititi, kakaka, kukuku? Mnakumbuka?

Yaliponyamaza tukadhani sasa mambo shwari, umeme wa kumwaga.

Kiko wapi? Ikaja korona tukapambana ikatulia, leo hakuna avaaye barakoa, anawaye maji tiririka na sabuni, ajitengaye na mikusanyiko. Tunadhani haipo, ngoja irudi tutatafutana walahi. Ni hayo tu.

**Alamsiki!**

# Bodi yapewa mtihani upotevu wa mapato

Na Romana Mallya

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama ameipa mtihani Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kuhakikisha inashughulika na taasisi ambazo mifumo yake inaruhusu upotevu mkubwa wa mapato ya serikali.

Jenista ameieleza bodi hiyo kuwa bado kuna mianya ya matumizi mabovu ya fedha, hasa serikali za mitaa, hivyo ni wajibu wao kufanya ukaguzi kama mifumo inasaidia ama la.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa bodi hiyo, Waziri Jenista aliitaka katika kutekeleza majukumu yake, ijiepushe na rushwa pamoja na makundi yenye nia mbaya ya kuharibu mwenendo mzima wa serikali mtandao.

Aliitaka bodi hiyo iliyo chini ya Mwenyekiti Dk. Musa Kisaka iangalie kuwapo mifumo ambayo ni jumuishi.

"Zipo taasisi zinatengeneza mifumo ambayo haifiki mwisho na hiyo inaruhusu sana upotevu mkubwa wa mapato na utoaji wa huduma ambao haukidhi vigezo kwa wananchi. "Zipo baadhi ya taasisi zina mifumo ya aina hii na hivyo kusababisha taratibu nyingine za utendaji kazi katika taasisi hizo, zifanyike nje ya mfumo ni jambo gumu, haiwezekani, kuweni wakali mwenyekiti.

"Kila taasisi inapojenga mfumo, unatakiwa kukamilika, hakuna sababu ya taasisi inakuwa na shughuli nyingine zinafanyika nje ya mfumo na nyingine ndani ya mfumo, hapana," aliagiza.

Aliwakumbusha kuwa vikwazo vingi vitakavyojitokeza kwa wadau mbalimbali ni wajibu wao kuzifanyia kazi kwa haraka. Waziri huyo oia alisema ni lazima wasimamie ongezeko la tishio la usalama wa mitandao ambayo yanajitokeza kila siku.

"Ninajua eGA wapo hapa saa 24 wakiangalia tishio gani na kulitafutia ufumbuzi, na ninyi bodi mlifanyie kazi usiku na mchana," aliagiza.

Alikumbusha kuwa mfumo wa watumishi na mishahara umejengwa na vijana wazawa na kwamba serikali inachotaka ni kuhakikisha wanawasomesha wengi zaidi ili wawe wabobevu katika mifumo.

"Tunao wengi lakini mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano(TEHAMA) inabadilika kila siku, tunatakiwa kutengeneza timu ya watu wenye uwezo wa kubadilika na teknolojia, mtusaidie tupate vijana wa kitanzania tupeleke huko nje wakasome," aliagiza.

Alisema bodi hiyo inaanza kazi katika kipindi ambacho uhitaji wa serikali mtandao ni mkubwa.

"Mafanikio ya serikali mtandao yapo, yalitoka kwenye serikali wakala mpaka serikali mtandao," alisema waziri huyo.

Mkurugenzi wa eGA, Benedict Ndomba aliahidi kutimiza maelekezo na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa bodi hiyo ili wafikie lengo kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya serikali mtandao na kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya serikali mtandao.

Alisema mamlaka imeendelea kusimamia na kuhimiza uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya serikali mtandao katika taasisi za umma ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi za mifumo, kufuatilia usalama mtandao, kushughulikia viashirikia vya matishio ya kiusalama mtandaoni, kutoa msaada wa kiufundi na kufanya utafiti na mafunzo.

Mwenyekiti mpya wa bodi hiyo, Kisaka alisema watajitahidi kufanya kazi kwa uwezo na weledi kusimamia serikali mtandao na kutekeleza majukumu wanayopewa.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akisalimiana na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, baada ya kuwasili katika mahafali ya 14 ya Chuo kikuu kishiriki cha Elimu cha Mkwawa, wilayani hapa mapema wiki hii. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Afrika Kusini yapongeza ulinzi maeneo ya historia

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI ya Afrika Kusini imeipongeza Tanzania kwa kuendelea kuhifadhi na kulinda maeneo ya historia ya wapigania uhuru wa nchi hiyo yaliyoko Mazimbu na Dakawa mkoani Morogoro.

Naibu Waziri wa Michezo, Sanaa na Utamaduni wa Afrika Kusini, Nocawe Mafu alitoa pongezi hizo juzi wakati wa mdahalo wa mashuhuda wa wapigania uhuru wa nchi hiyo.

Alisema Afrika Kusini na Tanzania ni ndugu, akikiri kushuhudia namna watanzania wanavyoenzi wapigania uhuru hao ambao waliishi nchini.

"Sisi na Tanzania ni ndugu, tumefurahi kuona mnavyotunza na kulinda maeneo ya urithi wa ukombozi wa bara letu na zaidi kwa nchi yetu. Tunawaahidi makubaliano ya ushirikiano wetu yote tutayatekeleza," alisema Nocawe.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Alberto Msando alisema nchi hizo zinashirikiana katika sekta nyingi kuwaenzi waasisi wake, Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Nelson Mandela.

Msando alitumia nafasi hiyo kuwaongoza Naibu Waziri huyo, Balozi wa Afrika Kusini nchini, Nolurthando Malepe na raia wa Afrika Kusini kutembelea kambi ya wapigania uhuru wa nchi hiyo na makaburi walikozikwa mashujaa waliopigania uhuru wa taifa hilo.

Tamasha la Utamaduni wa Afrika Kusini na Tanzania lilianza rasmi Novemba 18 na litafikia tamati Desemba 4 mwaka huu, likiwa na lengo la kuimarisha uhusiano katika sekta za utamaduni, sanaa na michezo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa Ushirikiano katika Sekta ya Utamaduni uliotiwa saini mwaka 2011.

Kambi ya wapigania uhuru ya ANC ya Dakawa ina makaburi 54 wakati Kambi ya Mazimbu ina makaburi 97 na kati yake, mawili yalifukuliwa mwaka 2004 na 2006 na mabaki yake kupelekwa Afrika Kusini.

## Manispaa yamulika usafi katika fukwe

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Meya Manispaa Wilaya ya Temeke, Anord Peter, amewataka wananchi kujenga utamaduni wa kusafisha fukwe akisisitiza uchafuzi wa fukwe unaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko.

Kiongozi huyo alitoa rai hiyo juzi wilayani Temeke, Dar es Salaam wakati wa hafla ya usafishaji fukwe iliyoandaliwa na asasi za TCCI na WAUMATE kwa lengo la kuunga mkono mikakati ya serikali kulinda mazingira.

Alisema usafi ni wajibu wa kila mtu na ni sehemu ya kuboresha afya, hivyo kila mwanajamii kwa nafasi yake anapaswa kufanya hivyo bila kusukumwa na mtu yeyote.

"Ninachotaka kuona Temeke inakuwa safi kila mahali, tunataka kuweka historia katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwa namba moja kwa usafi ili wengine waige mfano kwetu.

"Ukiangalia ufukwe huu ulikuwa mchafu sana, lakini leo (juzi) umesafishwa, unavutia hata mtu kuja kukaa hapa na kufaidi hali ya hewa, lakini pangekuwa pachafu, hakuna ambaye angependa kuja kupatumia.

"Katika wilaya hii kila mtu anapaswa kulinda eneo lake kwa kufanya usafi, hatupendi tupite sehemu tuone pachafu, ikifikia hatua wananchi hawaelewi sisi tutachukua hatua kwa sabau jambo la usafi kila siku Waziri (Dk. Seleman) Jafo analizungumza," alisema.

Balozi wa Mazingira, Richard Kalongola alisema nchi kwa sasa inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi, hivyo jamii haina budi kutunza mazingira na vyanzo vya maji.

"Tunawashukuru TCCI (taasisi inayojihusisha na usafi wa mazingira) kwa kuamua kungana na wakazi wa Temeke kusafisha fukwe, ni ukweli usiopingika fukwe nyingi zina uchafu mwingi sana, inapotokea taasisi inaunga mkono juhudi za serikali, sisi tunajisikia raha sana.

"Ukiangalia kipindi hiki nchi inakumbana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, tujiepushe na kukata miti ovyo, lakini tuendele kujenga utamaduni wa kusafisha mazingira yanayotuzunguka.

"Ukienda kwenye fukwe nyingine unakuata watu wamekaa wanafurahi kwa sababu mazingira yanaruhusu, ni safi. Kwa hiyo, niwaombe watu wa Temeke, jengeni utaratibu wa kusafisha mazingira.

"Nimesikia malalamiko kwamba wavuvi wanaotumia fukwe wanapenda sana kufanya usafi lakini tatizo vifaa, hili ninalibeba, tunakwenda kulifanyia kazi," aliahidi.

# MAISHA

NOVEMBA 27, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 14


## Makange ya nyama



Fahamu haya kabla ya kuuza nyumba

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15




## KATUNIKA

Ukurasa 16


# MAFUTA YA NAZI


## Ndevu murua zinazong'ara



Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | S | H | A | K | A |
| ■ | H | ■ | ■ | O | ■ |
| L | I | A | ■ | K | ■ |
| ■ | N | ■ | T | O | A |
| ■ | D | ■ | ■ | T | ■ |
| T | A | M | B | O | ■ |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
MWA, INA, SAUMU, LAANA, NYUNGU, LAWAMA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

MPAKE RANGI YA NJANO, KIJANI NA NYEKUNDU ILI NDEGE WETU APENDEZE



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO Juma alikuwa akimsaidia mama yake kuokota kuni katika pori jirani na nyumba yao. Wakati wanaendelea kukusanya kuni, Juma alimuuliza mama yake.

Juma: Eti mama msemo kila kijani una mti wake una maana gani?

Mama: Mwanangu una maana tofauti, lakini ninayojua ni kwamba kila kitu kina asili yake.

Juma: Kwani hakuna jani bila mti?

Mama: Mwanangu hilo haliwezekani, sawa na mtoto bila wazazi hilo ni jambo gumu

SWALI
Zao la korosho linalimwa mikoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO



Na Flora Wingia

# Nililazimisha kuoa kumbe ni dada!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na kashkash zinazojiri kwenye familia zetu kila uchao. Kumbuka Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita niliahidi kukuletea mifano ya vijana wanaozama kwenye mafanikio, kumbe ni ndugu hawapaswi kuoana. Hata wakilazimisha baadaye huzua balaa.

Wazazi ni walezi na washauri wazuri wa vijana wao. Hilo ni jukumu lao kwani wao ndio wasimamizi wakuu wa familia. Na wanapotekeleza jukumu hilo, vijana wanapaswa kuwa wasikivu kwani na wao (wazazi) wamepitia maisha hayo. Ndio maana wanaweza kuwashauri ili wasipoteze mwelekeo wa maisha.

Pale wazazi wanapokushauri, sikiliza kwa makini, usiwabeze na kuwadharau. Usiwaweke kando na kutafuta ushauri kwa watu wengine ambao ni maarufu kwako. Hatukatai kupata ushauri kwa watu wengine lakini wazazi wako nafasi yao ipo pale pale haiwezi kuchukuliwa na mtu mwingine.

Mara nyingi sana vijana wengi hasa wale ambao hawajaoa au kuolewa, hupata changamoto fulani kipindi kile ambacho wanataka kuanza maisha. Hii imekuwa ni changamoto sana kwenye familia nyingi.

Kijana anapofikiria kuoa anasema nimwambie baba au mama ya nini? Lakini kijana anakuja kuwaambia wazazi wakati ameshakutana na msichana huko chuoni na kwamba anataka aruhusiwe kuoa. Taarifa anaitoa wakati ameshakamilisha kila kitu.

Baba akimhoji kulikoni haraka kiasi hicho, kijana anang'aka na akikatazwa anasema kama ndivyo atajiua. Hivi kwa nini kijana kama huyu asimsikilize mzazi anachomshauri? Yaani ajiue wakati baba kamshauri jambo jema?

Vijana wanapaswa kutulia na kutafakari kwanza pale mzazi anapowashauri. Jiulize unataka nini katika hicho unachoking'ang'ania wewe. Siyo kwamba wanakushauri kwa mabaya. Hapana. Ipo sababu na hatari wanayoiona mbele yako!

Vipo vitu vya kuangalia na vya msingi sana katika maisha yako wewe kijana. Moja ni kusikiliza ushauri wa wazazi wako. Ipo mifano mingi ya vijana waliopuuzia ushauri wa wazazi wakajikuta wanaangukia pabaya. Kama yule binti daktari niliyemjadili wiki kadhaa kwa kumdharau mama yake akaishia kula jalalani.

Yupo kijana mmoja alitamani sana kumuoa binti fulani. Lakini baba yake akamkataza kwa sababu alipodadisi alimfahamu huyo binti. Ukiona mzazi anamkataza mwanae kuhusu jambo fulani, ujue ameona mbali.

Unaweza kuona kuwa anakuzibia riziki kwa yule umpendaye, kumbe wanakusaidia na kukuepusha na hatari ya baadaye, hivyo tafakari!

Sasa huyu kijana akang'ang'ania, na baba akasema haitawezekana. Kijana akasema nimeshaamua, nitaenda kuoa. Baba alikuwa anamkatalia kijana kuoa binti yule kwa sababu ni mtoto ambaye alimzaa nje ya ndoa lakini ikawa ni siri yake.

Wazazi wakamsihi asimuoe lakini kijana akaamua kutoroka naye kwenda mjini. Huko wakaendelea na maisha kwa takriban miaka 15. Hilo halikuwa jambo jema kwa kijana kudharau ushauri wa baba yake. Ni kweli Mungu anatoa baraka na kila kitu. Na kwamba, baraka zetu sisi zinatoka kwa wazazi wetu.

Kwa hiyo, yule kijana akaendelea kuishi kule mjini lakini hayakuwa maisha halisi kwani badala ya kuishi maisha ya kiuhalisia ya mume na mke, walikuwa wakiishi kama kaka na dada.Huyo anayemuita mke wake alikuwa ni mtoto ambaye baba yake alimzaa nje ya ndoa!

Wazazi hawakuwaona kwa miaka 15 na kila wakiulizia wanaambiwa wamehamia mji mwingine. Walikuwa na maisha ya kuhangaika huku na kule kwa kuwa hayakuwa maisha halisi ya ndoa.

Kijana unapaswa mzazi akubariki kwa jambo wanaliona ni jema. Ni muhimu wakutakie kheri na baraka ili ufanikiwe. Lakini vijana wengi hasa wanaofikia kipindi cha kuoa au kuolewa, wanakuwa na changamoto sana kusikiliza ushauri wa wazazi wao.

Inafikia wakati wazazi pia wanamkataza binti, asiolewe na kijana fulani. Binti anasema kama ni hivyo, nitakimbilia porini kujiua. Yaani ukajiue kwa ushauri wa wazazi? Hebu fikiria kabla ya kuamua, waza wazazi watakufikiriaje!

Wazazi wengine wanaweza wakashikamana na kusema, "haya nenda kajiue, kwani wamekufa wangapi...unataka kututishia maisha? Chukua kamba hii kajiue, ila andika uamuzi wako kwa maandishi polisi wasitusumbue."

Binti akakimbilia porini kujiua. Huko akakutana na simba akarudi mbio na kuwaangukia wazazi, na kuomba msamaha. Mfano mwingine wiki ijayo.

**Una kisa? Ujumbe 07268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI



Na Salome Kitomari

# Wanaume jitokezeni kueleza ukatili mnaofanyiwa na wake,wapenzi wenu

WIKI iliyopita Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima, alisema serikali imekuja na mifumo saidizi ya kuwawezesha wanaume kuripoti vitendo vya ukatili wanavyotendewa na wake zao au wapenzi wao.

Alisema kwa sasa wamebaini wanaume wengi wanapitia ukatili kwenye ngazi ya familia na jamii lakini kwa sababu hakukua na mfumo wa kuripoti wamejikuta wanaendelea kuumia bila msaada.

Alisema mifumo hiyo itasaidia wanaume kusema madhila wanayopitia, kwa sababu imeonekana matukio mengi ya ukatili wa kijinsia yanatokana na uvumilivu kufika mwisho na kutaka kuonyesha mamlaka au misuli aliyonayo.

Kwa sasa ukatili wa jinsi umeongezeka kiasi kwamba kila siku kuna tukio la mtu kumuua mpenzi wake, kumjeruhi au kufanya lolote baya na chanzo kikielezwa ni wivu wa mapenzi.

Waathirika wakubwa ni wanawake na watoto kwa sababu anayevumilia huamua kushusha hasira yake kwa wanaomzunguka au waliomfanyia jambo lolote ambalo mbele ya jamii ameona amedhalilishwa.

Mwanaume amelelewa na jamii kama mtu wa kuvumilia,kutoonyesha machozi au maumivu yake mbele ya jamii kwa kuwa kufanya hivyo ni kuonyesha udhaifu wakati mwanaume ni mwenye misuli na nguvu nyingi.

Tupo kwenye maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili,ni muhimu kujumuisha jamii yote ili tuwe na kizazi endelevu na kinachoishi kwa amani na utulivu.

Mathalani, kwenye jamii inapotokea msiba mtu kaondokewa na mtu wake wa karibu sana anashindwa au kuzuiwa kulia huku akiambiwa yeye ni mwanaume hapaswi kuonyesha maumivu.

Pia programu nyingi zimeandaliwa kuwawezesha wanawake ambao kimsingi waliachwa nyuma na kunyanyaswa kiuchumi lakini kwa sasa wanawezeshwa kiasi kwamba wengi wanaweza kujisimamia kimaisha.

Wanaume watumie vyema mfumo huo ili tuwe na jamii yenye usawa kwa kuwa nao ni binadamu kama wengine wana haki zote za msingi.

Kwenye jamii yetu tunaona matukio mengi ya udhalilishaji wa watoto wa kiume ambayo lazima yachukuliwe hatua mapema,programu za uwezeshaji wanaume na wanawake ziwe endelevu na saidizi.

Hivi karibuni, mwanaume mmoja alihojiwa na chombo kimoja cha habari akieleza kwa uwazi madhila anayoyapitia kwa kuteswa na mkewe, alisema anapigwa sana na mara kadhaa wameenda kanisani wakaambiwa ndoa ni hadi kifo kiwatenganishe,kasoro zinazojitokeza washirikiane kuzitatua.

Hii inaonyesha kuna tatizo kubwa kwenye jamii ambalo lazima liangaliwe,kwamba tunavyowekeza nguvu kumwezesha mwanamke na mwanaume naye asiachwe nyuma.

Ni muhimu mpango kazi wa taifa kwenye eneo la uwezeshaji likajumuisha wanawake na wanaume, itasaidia kuwa na kizazi chenye usawa wa kijinsia.

Ni vyema kukawa na majukwaa ya wanaume kujadili ukatili wa kijinsia kwenye ngazi ya familia na mitaa,kwa kuwa jamii inayozungumza ndio yenye uhai.

Kuelewa madhila anayokutana nayo mtu sio udhaifu na hakutaondoa uanaume wake,bali ni namna pekee ya kuuponya moyo na akili yake.

Wanaume kwenye mtaa fulani wanaweza kuamua kuwa na vikao vya kila mwezi kuzungumza hali ya usawa wa kijinsia, lakini pia kufundisha vijana namna ya kuwa wanaume wawajibikaji na wajenzi wa familia.

Kwa kuzungumza kutasaidia watu kueleza hisia zao na kupunguza maumivu waliyonayo kwa kuwa inaaminika kwa kuzungumza mtu anatoa dukuduku na pia ni tiba nzuri kwa moyo unaoumia ndio maana nchi nyingine duniani kuna mahali pa kwenda kufunguka yote ya moyoni alafu unarudi nyumbani ukiwa umetua mzigo.







Ilikuwa siku ya furaha kwa familia ya Bwana Kelvin Komba, wakati wakimuaga binti yao mpendwa Dk. Josephine Komba, katika sherehe iliyofanyika Oktoba 22, wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma.









# MITINDO





# YA KALE DHAHABU

KILA siku kunaibuka mitindo mingi mipya ya mavazi, lakini kuna aina ya mitindo ya zamani bado inaendelea kudumu kutokana na kupendwa na watu.

Makoti aina ya Duffel, ni baadhi ya mtindo inayoendelea kutumiwa na kizazi cha sasa, licha ya vazi hilo kubuniwa zamani.

Vazi hili linalovaliwa na wanaume lilianza kutumiwa na askari wa ufalme wa Uingereza, lakini kutokana na mwonekano wake lilisambaa kwa kasi na kupendwa na watu wengi.

Aina hii ya kanzu ina vifungo kati ya vitatu hadi vinne vinavyojulikana kama 'Walrus' ambavyo vimefungwa na vifungo vya ngozi au kamba.

Katika mitindo ya kisasa koti hili refu huzidi kidogo kiunoni, kupunguza urefu wake wa awali ambao hufikia magoti.

Baadhi ya vitu vinavyoambatana kwenye koti la Duffel ni kuwa na kitambaa kigumu kisichoruhusu maji mabegani, kichupa cha kitufe kwenye shingo, lebo kwenye mikono, mifuko ya nje na mikunjo inayoruhusu kusogezwa.

Vazi hili lenye mtindo wa kisasa linafaa kuvaliwa katika sehemu tofauti kutokana na unadhifu wake.





UREMBO

Na Mary Geofrey





# MAFUTA YA NAZI

## Ndevu murua zinazong'ara

MAFUTA ya nazi yana faida nyingi kwa matumizi ya utunzaji wa ndevu.

Aina hii ya mafuta huzuia ngozi kuwasha, kuimarisha nywele, kuboresha muonekano na kuweka ngozi kwenye hali ya unyevu.

Mafuta ya nazi hutumiwa katika masuala yote ya urembo, kama utunzaji wa ngozi, kupambana na kuzeeka hadi kupunguza uzito.

Pia yanatumika kama kiungo kinachotumika sana katika bidhaa za urembo na nywele.

**NAMNA YA KUTUMIA**

Tafuta mafuta ya nazi ambayo ni mazito ambayo yanaweza kuwa ghali zaidi kutokana na ubora wake.

Tumia kiasi kidogo cha mafuta haya na ueneze kwenye vidole vyako, kisha paka mafuta kwenye ndevu zako, kuhakikisha kuwa inafikia kiwango cha chini cha ndevu zako, haswa ngozi iliyo chini ya ndevu.

**FAIDA ZAKE**

Moja ya shida kuu ya ndevu ni kukatika na kuharibika ubora wake.

Mafuta ya nazi husaidia kuondoa tatizo hili na kufanya ndevu zako kuwa na afya na kuota katika mpangilio mzuri.

Paka mafuta katika ndevu zako kila baada ya kuoga au kusafisha uso na maji.

Pia hupunguza muwasho kwenye ngozi kutokana na kunyoa, haswa kwa wenye ngozi laini, unaweza kutumia mafuta ya nazi kwenye ngozi kabla na baada ya kunyoa. Hii inaweza kuongeza uponyaji pale unapojikata katika harakati za unyoaji.

**KUIPA NGOZI UNYEVU**

Sote tunajua umuhimu wa unyevu katika ngozi na ukuaji wa nywele, ni sehemu pia katika ukuaji wa ndevu na ngozi.

Hasa baada ya kunyoa au kutumia wembe kusafisha kingo zako, tumia mafuta ya nazi kuzuia uvimbe au wekundu.

Hufanya ngozi na ndevu kubaki kuwa na unyevu na kuupa ukuaji wake kuwa bora na ndevu kuonekana bora.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Makange ya nyama

ROSTI ya aina hii unaweza kuitumia kwa ajili ya kuku, samaki, nyama lakini jambo moja muhimu ni kuhakikisha unaongeza kiungo kimoja.

Kama unapika samaki utaongeza fish masala au Chicken masala kama unapika kuku, vilevile kama unapika nyama basi utaongeza bifu masala.

**MAHITAJI**

Nyama, kitunguu, nyanya, karoti, hoho, soya sauce, tangawizi na Kitunguu swaumu.

**NAMNA YA KUPIKA**

Chemsha nyama hadi iive vizuri kisha kata vipande vidogovidogo kwa urefu, chukua mboga zote zikate kwa urefu.

Sifa kubwa ya makange ni kwamba mboga hazitakiwi kuiva sana hivyo katika kuanza kupika unaanza kama ifuatavyo.

Chukua sufuria weka jikoni, kisha weka mafuta kidogo sana, mafuta yakipata moto weka vitunguu maji na tangawizi pamoja na kitunguu swaumu, kumbuka vitunguu havitakiwi kuwa kahawia, hivyo baada ya kuweka karoti inafuatia, kisha hoho, nyanya na nyama.

Weka soya sosi kiasi kisha pika kwa kugeuza, baada ya sekunde kadhaa makange yatakuwa tayari unaweza kuepua jikoni na tayari kwa kuliwa na wali, chipsi, ugali au chakula kingine unachopendelea.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Fahamu haya kabla ya kuuza nyumba

BIASHARA ya nyumba na uwekezaji wa majengo ya kisasa inaendelea kushika kasi kila siku.

Mshauri wa uwekezaji masuala ya majengo, Abedi Charles, anasema kabla ya kuuza nyumba ni bora ufanye tathmini, lengo na sababu ya kufanya hivyo ili uamuzi uwe sahihi.

Miongoni mwa mambo ya kuzingatia kabla ya kufikia uamuzi wa kuuza nyumba ni lazima utathmini lengo au sababu kuu ya kufanya hivyo.

Anasema wakati tulionao biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo unafanyika kwa mbinu za kisasa ambazo ni matokeo chanya ya ukuaji wa sekta hiyo ya ujenzi inayotokana na mapinduzi ya teknolojia mbalimbali duniani kote.

"Watu binafsi, kampuni na taasisi nyingi zimejitokeza kwa wingi kuzitumia fursa zinazoendelea kujitokeza kila siku kwenye biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo husussani kwa kuiendesha kisasa zaidi kwa kutoa huduma za makazi na biashara kwa wadau mbalimbali,"anasema Charles.

"Lakini kuna baadhi ya watu wamejikuta wakiingia kwenye uuzaji wa majengo yao kutokana na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo kwenye maisha, na ndiyo maana ninashauri kwamba ni muhimu sana ukajitathmini kabla ya kuuza nyumba yako, je ni kwa lengo la kibiashara au kutokana na kushindwa kukabiliana na msukosuko wa changamoto za maisha zinazokukabili."

"Kutulia na kujitathmini kutakusaidia ufikiri vizuri na wakati mwingine kuepuka majuto kama hukuwa na ulazima wa kuuza nyumba yako."



Jambo jingine anasema kabla ya kufanya uamuzi huo wa kuuza nyumba ni vema kutathmini bei na gharama ya mauzo ambayo unayapeleka sokoni ili kukusaidia kufahamu kiwango halisi na faida au mapato utakayopata kwa kutimiza malengo unayokusudia.

Mtaalam huyo anashauri kwamba ni muhimu kuzingatia kwa kuhakikisha nyumba yako inakuwa na muonekano mzuri na kushawishi wanunuzi, na kwamba kama rangi yake ilikuwa imechakaa ni vema kuipaka upya pamoja na kuzingatia kuwa inakuwa safi wakati wote.

Anasema mvuto wa nyumba nao utakusaidia kukuongoza pia katika namna ya kufanya tathmini ya bei na itasaidia inunuliwe kwa muda mfupi.

Pia, anashauri kwamba kabla ya kufanya uamuzi wa mauzo, ni vema kutathmini hali ya soko la nyumba na si kukurupuka.

## Namna ya kuweka vizimba vya maua mbele ya nyumba



BAADHI ya watu wanapenda kupamba nyumba zao kwa urembo tofauti.

Hata hivyo, upambaji wa nyumba kwa kujenga vizimba maalum vya majani na maua unaweza kukupa mwonekano wa kipekee.

Nyumba iliyo na vizimba pembeni ya ukuta kwa ajili ya kupanda maua ya majini, hufanya iwe na mwonekano maridadi na unaovutia.

Zifuatazo ni baadhi ya hatua unazotakiwa kuchukua kwa ajili ya kuandaa vizimba vya maua.


1: Andaa vizimba mbele ya nyumba, eneo la kuegesha magari au sehemu ya kuanikia nguo kulingana na mtindo unaoona unafaa.

2: Weka udongo wenye rutuba kwa ajili ya kufanya majani na maua kustawi vizuri.

3: Panda majani ya ukoka wa kijani na maua kwa mpangilio maalum na kumwagilia maji mara kwa mara.

4: Majani na maua yakianza kustawi, hakikisha unakata vizuri kwa ku tumia mashine au mikasi kwa mitindo unayoitaka.

# KATUNI




...KINYUNYIZO CHA LEO...

RAHA YA MECHI MAGOLI...

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Putin ahisi maumivu vifo vya wanajeshi wake

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia amesema anahisi maumivu kama wanavyojisikia kundi la wanawake ambao watoto wao wanapambana katika vita ya Ukraine.

"Nahisi maumivu, hakuna kitu chochote kinachoweza kulinganishwa na kumkosa mtoto wako wa kiume",alisema Rais Putin wakati akizungumza na kundi hilo la Wanawake.

Kundi la wanawake hao ni wajumbe wa vuguvugu linaloungа mkono utawala wa Russia.

Hata hivyo, wakosoaji walisema akina mama hao walichaguliwa kwa uangalifu.

Ndani ya Russia, upinzani dhidi ya uvamizi wa Ukraine umekuwa ukiendelea kuongezeka.

Makundi ya wanawake hao wamekuwa wakilalamika wazi kwamba watoto wao wa kiume wanapelekwa katika vita huku wakiwa na mafunzo duni ya kijeshi na hawapewi silaha zinazofaa na nguo.

Baadhi pia walilishutumu jeshi la Russia kwa kuwageuza wale waliolazimishwa kuingia vitani kama vifaa vya kutumiwa, kufuatia kushindwa vibaya kwa jeshi katika miezi ya hivi karibuni.

Wanajeshi wapatao 100,000 wa nchi hiyo na idadi kama hiyo wa Ukraine wameuawa au kujeruhiwa tangu vita hivyo vilipoanza Februari 24.

Katika taarifa iliyotolewa na Marekani, inaeleza kuwa Russia ilikiri kuwa katika mwezi Septemba makosa waliyoyafanya ni kuwaingiza jeshini wanajeshi wa akiba.

Katika mkutano wa juzi uliofanyika katika makazi yake ya kitaifa yaliyopo karibu na mji mkuu Moscow, Putin alionyeshwa akiwa amekaa kwenye meza moja na kikundi cha akina mama 17.

Baadhi yao walikuwa wamevaa vitambaa vyeusi kichwani kama ishara ya kuomboleza.

"Ninataka ninyi mjue kuwa mimi mwenyewe binafsi, na uongozi wote wa nchi, tunahisi maumivu haya ," alisema kiongozi huyo.

Aliwaambia mama mmoja kuwa mwanaye wa kiume alikuwa amefikia lengo lake na hakufa bure.

Putin alisema kuwa alitaka kukutana na wanawake hao ana kwa ana kusikiliza kutoka kwao wenyewe kuhusu hali ya mambo katika maeneo yao.

Alifichua kuwa mara kwa mara amekuwa akizungumza moja kwa moja na wanajeshi wa Russia walioko katika uwanja wa mapigano.

Kiongozi huyo pia aliwataka akina mama hao kutoamini taarifa feki na uongo kuhusu vita vinavyoendelea kwenye televisheni na intaneti.

Katika taarifa kuhusu mkutano huo iliyochapishwa na ofisi ya Rais saa kadhaa baadaye, baadhi ya wanawake walitambuliwa kama wanawake ambao ni sehemu ya vuguvugu linalomuunga mkono Putin.

Wanawake hao walikuwa kutoka sehemu mbali mbali za nchi hiyo, ilisema taarifa hiyo.

Mjumbe wa kundi la All-Russian Popular Front linaloungwa mkono na utawala wa Russia pia alikuwepo pamoja na washiriki kutoka Shirika la Combat Brotherhood , ambalo hukusanya misaada ya kibinadamu kwa ajili ya wanajeshi wa Russia.

Wakati huo huo, Ofisi ya rais wa Ukraine ilisema Russia itawajibika kuwalipia wahanga wa njaa ya enzi ya Sovieti iliyosababisha vifo vya mamilioni ya watu katika majira ya baridi kati ya mwaka 1932-1933.

Mkuu wa utawala kwenye ofisi ya rais Andriy Yermak, aliandika jana kwenye mtandao wa Telegram kwamba Russia itawalipa wahanga wote wa Holodomor na itajibu kuhusu uhalifu inaoufanya sasa.

Ameandika hayo katika siku ya maadhimisho ya kumbukumbu ya wahanga wa Holodomor yaliyofanyika jana.

Novemba, 1932 kiongozi wa Kisovieti Joseph Stalin aliwaruhusu polisi kukamata nafaka na mifugo katika mashamba ya pamoja ya Waukraine ikiwa ni pamoja na mbegu ambazo wangezitumia katika msimu ujao na kusababisha raia wengi kufa kwa njaa.

**BBC**



Rais wa Russia, Vladmiry Putin, akizungumza na wanawake ambao watoto wao wanapigana nchini Ukraine juzi. **PICHA: REUTERS**

# China iko tayari kushirikiana na Kim

**PYONGYUNG,** KOREA KASKAZINI

RAIS wa China Xi Jinping amemuambia kiongozi wa Korea Kaskazini Kim Jong Un kwamba yuko tayari kushirikiana naye kuleta amani ulimwenguni.

Taarifa hiyo ni kulingana na vyombo vya habari vya serikali ya Korea Kaskazini iliyotolewa jana.

Ujumbe huo wa Xi unatolewa siku chache baada ya Korea Kaskazini kufyatua kombora la masafa marefu katika moja ya majaribio yake makubwa ya hivi karibuni yaliyoongeza wasiwasi kwamba inajiandaa kufanya jaribio lake la saba la nyuklia na la kwanza tangu mwaka 2017.

Kwenye ujumbe wake Xi alisema yuko tayari kushirikiana na Korea Kaskazini katika kuleta amani, utulivu, maendeleo na ustawi wa kikanda na ulimwengu kutokana na mabadiliko yanayotokea kinyume na matarajio kuanzia ya nyakati hadi kihistoria.

**DW**

# Somalia yatangaza vita na al-Shabaab

**MOGADISHU,** SOMALIA

SERIKALI ya Somalia imetangaza vita kamili dhidi ya wanamgambo wa Al-Shabaab na kuidhinisha juhudi kadhaa za kupambana na ugaidi.

Licha ya mafanikio yake ya kijeshi ya siku za mwanzo, huenda vita hivyo vikawa vigumu na vya muda mrefu. Kundi hilo lenye mafungamano na al-Qaeda lilifukuzwa kwenye miji mikubwa ya Somalia muongo mmoja uliopita lakini bado linashikilia maeneo mengi ya mashambani ambako makundi ya wanamgambo yameungana na kupambana na uasi wa kundi hilo.

Koo mbili katikati mwa Somalia zilizochoshwa na utawala wa Al-Shabaab, zilianzisha uasi dhidi ya kundi hilo mwezi Julai uliosambaa haraka katika mikoa ya Hirshabelle na Galmudug na mwezi Septemba ulipata usaidizi wa makomandoo waliopewa mafunzo na Marekani na Jeshi la Kitaifa la Somalia.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Migogoro, ICG, Omar Mahmood amesema nia ya serikali ni kuendeleza kasi ya sasa na kuhimiza uasi kama huo katika maeneo yote yanayoshikiliwa na Al-Shabaab nchini Somalia.

**DW**

# Vigogo wa CHADEMA wapaa Ulaya kusaka uungwaji mkono

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI waandamizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wako ziarani barani Ulaya kwa siku saba kwa lengo la kutafuta uungwaji mkono katika jumuiya za kimataifa kuimarisha demokrasia nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi na Mambo ya Nje, John Mrema, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu (pichani) anaongoza ujumbe huo katika ziara hiyo iliyoanza Jumatano.

Viongozi wengine katika ujumbe huo ni Katibu Mkuu, John Mnyika, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Mjumbe wa Kamati Kuu, Zeudi Mvano na Mwenyekiti wa BAVICHA Taifa, John Pambalu.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa ziara hiyo inahusisha nchi za Ujerumani na Ubelgiji ambako ujumbe huo utawasilisha wito wa kuungwa mkono katika mpango wa kupatikana kwa katiba mpya na tume huru ya uchaguzi, pia urudishaji wa haki za kufanya siasa ikiwamo mikutano ya hadhara na maandamano.



Taarifa hiyo ilibainisha baadhi ya taasisi ambazo CHADEMA itafikisha ujumbe wake zinajumuisha Chama cha CDU, Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo za Ujerumani. "Pia watawafikia wabunge wa Bunge la Taifa la Ujerumani, Bunge la Umoja wa Ulaya, Taasisi ya Kimataifa ya Uwazi (International Transparency), Taasisi ya Kimataifa ya Haki za Binadamu.

"Lengo ni kuhakikisha mazingira ya siasa Tanzania yanaimarika na katiba mpya na tume huru ya uchaguzi zinapatikana kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2025 ili kuhakikisha kunakuwapo uchaguzi huru wa haki na unaokubalika," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

CHADEMA pia imeziomba taasisi za kimataifa kutupia jicho siasa za Tanzania ili kudhibiti inachokiita kuirudisha nchi katika siasa kandamizi, uminywaji wa demokrasia na uvunjifu wa haki za binadamu kwa kile wanachodai kuna viashiria vimeanza kuonekana.

# Maelfu kuagana na kero uhaba wa maji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI 4,144 wa Kijiji cha Nyombo wilayani Njombe wanatarajiwa kuondokana na kero ya kufuata maji umbali mrefu baada ya serikali kutekeleza mradi wa maji safi na salama.

Mradi huo unatekelezwa na Kampuni ya Build Tech Eng unaogharimu zaidi ya Sh. milioni 800, sasa ukiwa umefikia asilimia 75.

Mkazi wa kijiji hicho, Anastazia Mbata aliiambia Nipashe jana kuwa kwa miaka mingi wamekuwa wakipata tabu kutokana na ukosefu wa maji safi na salama.

Alisema mradi huo utakapokamilika utawasaidia kuondokana na kero ya kufuata maji umbali mrefu na kutumia maji yasiyo salama.

"Mradi huu ukikamilika tutaneemeka kwa kupata maji safi kwa sababu maji ya mtoni si salama, unakuta hata mifugo inayatumia, wanawake tunapata tabu, tunatoka shambani halafu ukirudi nyumbani ukachote maji kisimani au mtoni," alisema.

Mkazi mwingine, Ezekia Mligula alisema: "Mpaka sasa hali ni mbaya kwa sababu tunatumia visima ambavyo wananchi wamejitolea kuchimba, maji mengi tunachota mtoni ambapo ni umbali wa kilometa moja au mbili."

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Njombe, Elikalia Malisa alisema kikwazo cha ukamilishaji mradi huo kilikuwa kuchelewa kwa malipo kwa mkandarasi.

Mkandarasi anayetekeleza mradi huo, Msafiri Mtyauli alimwomba mkurugenzi kumpatiwa fedha anazodai ili utekelezaji wake uwe kwa haraka kwa sababu amefanya kazi hiyo pasipo malipo.

Mkurugenzi Mkuu RUWASA, Clement Kivegalo alisema serikali itamlipa fedha hizo na kumtaka kukamilisha kazi hiyo ifikapo Desemba 25 mwaka huu ili sikukuu ya Krismasi wananchi wawe na maji safi.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Wanamuziki, waigizaji wanavyosaka 'limbwata' Ni kweli ipo, au haipo?



**Na Adam Fungamwango**

**Kama utamtendea mema, kumjali, kumsikiliza, kujua tabia yake na kuangalia nini anapenda na nini hapendi, ukaenda naye hivyo, sidhani kama hatoonyesha upendo. Wanaume ni kama watoto wadogo tu.**

HIVI kweli duniani kuna dawa ya mapenzi? Kuna watu wanaamini kuwa zipo dawa hasa za miti shamba ambazo zina uwezo wa kumfanya mpenzi wake ampende zaidi ya upendo wa kawaida.

Nikisema upendo zaidi ya kawaida nina maana nzito kidogo. Ni kwamba wote wanaosaka dawa za kuwapumbaza wapenzi wao mara nyingi kwanza wanaanza kupendwa. Halafu sasa wao hawataki kupendwa wanavyopendwa. Wanataka wapendwe zaidi ya kawaida. Yaani anayependa awe kama zezeta. Kila analoambiwa akubali. Na mara nyingi wanaopendwa wanakwenda kwa kina 'Kalumanzira' kwa ajili ya kuwapumbaza wapenzi wao wana sababu kuu mbili.

Kwanza ni kutaka udhibiti wa yeye awe peke yake, na wala mpenzi wake asiwe na hamu ya kutafuta mwingine.

Pili ni uwezeshwaji. Wanachotaka kile ambacho anakipata mpenzi wake basi asilimia kubwa kama siyo 80 mpaka 90 akipate yeye. Kisiende kwa mwingine wala kisibaki kwa mpenzi wake. Ukiangalia sana hizi zote ni dalili za ubinafsi.

Ukisikiliza nyimbo nyingi zinazoimbwa, filamu na tamthilia nyingi, na hata matukio mengi ya kijamii, yanaonyesha kuwa asilimia 90 au zaidi ya hapo, ambao huwa wanakwenda kwa waganga kusaka dawa za kuwapumbaza wapenzi wao ili wawapende zaidi ya wanavyowapenda ni wanawake.

Jamii imeipa jina dawa hiyo inaitwa 'limbwata'. Ukiutaja msamiati huo popote pale, utaambiwa kuwa ni dawa anayopewa mwanaume kwa ajili ya kudhibitiwa au 'kutiwa mikononi', asifurukute wala kutingishika.

Hapo mwanaume chochote atakachoambiwa na mpenzi wake yupo tayari, hata kile ambacho kwa wakati huo hana uwezo nacho, lakini atahangaika huku na huko hata kwa kukopa na kujitia madeni ili mradi akipeleke.

Kama nilivyotangulia kusema kuwa mambo haya yapo kwenye jamii na ndiyo maana wanamuziki na wasanii wanayaimba. Filamu na tamthilia nazo zinatuonyesha kuwepo na vitu kama hivyo. Tena mambo haya si Tanzania tu, bali yapo Afrika nzima mpaka bara Asia ambako nako tumekuwa tukitazama tamthilia zao. Nako 'limbwata' ipo kama kawaida.

Lakini swali linakuja, hivi kweli ni lazima kutumia dawa ili kumdhibiti mpenzi? Na kweli dawa hizo zinafanya kazi?

Mpaka sasa hakuna uthibitisho wa kisayansi unaoonyesha kuwa dawa hizo za mitishamba zinafanya kazi ya kumpumbaza mpenzi zaidi ya dhana. Hata hivyo ukweli unabaki pale pale kuwa baadhi ya wanawake wanafanya hivyo.

Na wanamuziki, waigizaji wote wanatuonyesha kuwa hayo yanafanyika, lakini mwisho wake unakuwa mbaya.

Kwa maana hiyo wanatuambia kuwa hakuna dawa ya mapenzi duniani. Dawa ya mapenzi ni mapenzi yenyewe.

Kama utamtendea mema, kumjali, kumsikiliza, kujua tabia yake na kuangalia nini anapenda na nini hapendi, ukaenda naye hivyo, sidhani kama hatoonyesha upendo.

Wanaume ni kama watoto wadogo tu. Ukiwachunguza watoto wadogo, ukatambua wanapenda sana kwenda kwenye nyumba fulani kucheza na nyingine hawapendi kwenda, utagundua wanayokwenda kuna upendo, mwenyewe anawakaribisha vizuri, anaweza kuwapa pipi na vizawadi vidogo, kuongea nao vizuri na mengine, lakini wanapopakwepa utagundua huwa wanakaripiwa, kusimangwa na kutolewa maneno yasiyofaa yakiwemo "hamna kwenu, mnachafua uwanja wangu." Naye mwanaume afanana na hivyo, kuwa mkarimu tu, hala haitaji 'limbwata.'

Wanamuziki wanasemaje kuhusu 'limbwata'? Mbaraka Mwinshehe Mwaruka alitunga wimbo uitwao 'Dawa ya Mapenzi' ambao mashairi yake ni hata hapa.

"Kwa nini unahangaika kutafuta dawa ya mapenzi kwa waganga. Madawa yasiyopimwa yaweza kumuumiza mwezio we mama. Kwanza jiulize kwa nini hupendeki siku hizi mama. Bembeleza bwana yako muishi pamoja usitumie dawa.

Hakuna dawa kabisa ya mapenzi duniani, na sasa hiyo utafutayo ya kumuua mpenzi wako. Kwanza chungua na kufikiri kwa nini sasa hupendeki, uzidishapo madawa mengi, ukiachika utafanyaje?

Wengine wengi walifanya hivyo kutafuta mabwana wawapende, matokeo yalikuwa vifo na hivi sasa ni wakiwa."

Tukiachana na wimbo huo, kuna mwingine ambao ulitungwa na John Simon akiwa na JKT Kimbunga Stereo uitwao 'Ushirikina'.

"Ingawa sumu ya ugonjwa ni dawa, lakini dawa zingine mbaya, ni za kupoteza uhai. Kuna msichana mmoja hapo zamani alimpenda mumewe, akaenda kwa mganga, kutafuta dawa ya mapenzi, akamlisha mumewe.

Bwana alipokula cha jioni hakutoka nje, asubuhi na mapema watu walikuta ameshakufa.

Maisha ya mumewe sasa yameshapotea oo jama, alivyotegemea, wala haikuwa hivyo alifanya vibaya sana.

Badala ya kupendwa sasa yamekuwa majuto anahangaika. Hilo ni fundisho kwa wanawake msifanye hivyo."

Nyimbo hizi zote zinaonyesha kuwa wapo baadhi ya akinadada hao. Na zipo dawa hizo, lakini zinaonyesha kuwa badala ya kutibu tatizo, zinakwenda kuzua tatizo lingine. Nalo ni vifo kwa wapenzi wao. Kuna wanaokuwa mazezeta kabisa.

Mbaraka anakuambia hakuna kabisa dawa ya mapenzi duniani. Dawa hapa ni kujiuliza kwa nini siku hizi hupendeki. Lifanyie kazi, jibu litakuja. Hakuna binadamu duniani asiyempenda mtu anayempenda.

HADITHI

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.

Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika-7

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Ni kweli mwanangu, hata mimi mama yako na baba yako tulikuwa na wazo hilo, lakini pesa yenyewe ya matibabu ya kumudu hilo hatuna, pili hili baba siyo la hospitali, ni michezo tu ya watu, wamemroga, kuna kijana alikuwa anataka kumuoa, akakataa, ndiyo mama yake akamfanya hivi."

"Sawa mama, mimi sitaki kuingilia masuala yenu mnayoamini, lakini mimi naomba tu apelekwe hospitali, akirudi mtaendelea kupelekana kwa waganga na suala la gharama mimi nitagharamia matibabu yote, hata wakisema alazwe mwezi mzima.

Mama Vajayo alipatwa na mshtuko kidogo. Hakutarajia hilo. Mtu ambaye hivi karibuni amefanyiwa kadhia kubwa kama ile, leo anajibebesha mzigo wa gharama.

Moyoni mwake hakutaka binti yake apelekwe hospitali kwa sababu aliamini amerogwa, lakini kutokana na heshima kwa kijana Jerry kuthamini mchango wake licha ya yote yale aliyofanyiwa na binti yake, akaamua kukubali.

"Sawa mwanangu, nimekubali."


Jerry aliwaangalia mzee Mbegu na Zulfa kwa zamu. Wote walitabasamu. Zulfa alionekana kupata imani ya kupona kwani alianza kukata tamaa ya kuishi.

Kazi ya kwanza iliyofanyika ni kwenda kukodi bajaj kwa ajili ya kumpeleka hospitali ya Tumbi. Mama Zulfa aliomba binti yake atolewe hapo kuanzia saa mbili usiku kwani hakutaka jioni ile kila mtu aone anavyoondoka.

Bado mama huyo aliendelea na imani yake ya kuwa ugonjwa wa binti yake ni wa kutengenezwa na nyoka aliyemuuma si wa kawaida, ni hila za mama Said na familia yake.

Muda ulifika, wakaondoka. Zulfa alifikishwa kwenye Hospitali ya Tumbi, baada ya vipimo ilionekana kuwa pamoja na kwamba sumu ambayo ingeweza kumletea kifo ilitoka, lakini kiasi kidogo kilichobaki kiliendelea kuutafuna mguu. Walichofanya ni kumpiga sindano ya kuondoa sumu kidogo iliyobaki mwilini, lakini pia kumuwekea dripu mbili za maji kwani alionekana kuwa na upungufu kutokana na sumu hiyo.

Baada ya siku mbili za kulazwa, madaktari walimpa rufaa ya kupelekwa kwenye hospitali ya Muhimbili, Dar es Salaam kwa ajili ya kuangalia mguu ambao ulianza kuleta athari kutokana na mabaki ya sumu kukaa na muda wa wiki kadhaa bila kutibiwa.




**"Huyu mgonjwa pamoja na kwamba amepata nafuu sana na anakwenda kumalizia dawa na mguu amerudi kwenye hali yake ya kawaida mimi sitaki kwanza arudi nyumbani."**

*********************************

Ilikuwa ni wiki ngumu kwa familia ya kina Zulfa kutokana na kuwa na ziara ya safari kutoka Kibaha na kwenda Muhimbili na kurudi.

Jerry alikuwa akiwawezesha usafiri mzee Mbegu na mama Zulfa pesa ya usafiri ya kwenda na kurudi kila siku mbali na pesa za matibabu.

Licha ya kufanya yote hayo, kitu ambacho alichojizuia Jerry ni kuulizia habari ya aliyetarajia kuwa mkewe Vayajo. Hakuonekana nyumbani na wala hakuonekana hospitali wakati mdogo wake anaumwa.

Si tu kwamba hakutaka kuwafanya wajisikie vibaya, lakini hakutaka pia kuumiza moyo wake ambao zaidi ya miaka kadhaa nyuma ulikuwa umevunjika kutokana na yote yaliyomtokea.

"Baba tunashukuru sana kwa yote uliyotutendea Mungu atakulipa na siyo sisi." Mama Zulfa aliongea kwa sauti ya upole baada ya kutolewa ruhusa na daktari kuwa sasa mgonjwa anaruhusiwa kuondoka, lakini akiwa nyumbani awe anatumia dawa alizopewa.

"Nashukuru mama, lakini nimefanya hivyo kama wajibu wangu." Akajibu Jerry.

"Baba sijui niseme nini, wewe ndiyo ulikuwa mkwe wangu wa kweli kabisa, ila tu yaliyotokea yametokea na Mungu ana makusudio yake." Ilikuwa sauti ya baba mzazi wa Vayajo.

"Usijali baba, yale yaliyotokea yamepita." Akajibu Jerry huku akiangalia chini.

Ukweli ni kwamba wazazi wa Vayajo waliona ajabu kwa mtu ambaye alikimbiwa na binti yao, leo kuwa msitari wa mbele kumuuguza kwa kumlipia gharama zote binti yao mwingine kitu ambacho kwa mwingine isingewezekana.

Walishindwa kung'amua kuwa Jerry alifanya yote hayo kwa sababu ya mzee Mbegu. Ndiye aliyemuomba aende kwa ajili ya kusawazisha mambo.

"Ila baba nina jambo moja la kukwambia." Mama alikuwa kama amekumbuka jambo. Kabla yoyote hajasema kitu akaendelea.

"Huyu mgonjwa pamoja na kwamba amepata nafuu sana na anakwenda kumalizia dawa na mguu amerudi kwenye hali yake ya kawaida mimi sitaki kwanza arudi nyumbani."

"Hata mimi nilikuwa na wazo kama hilo." Mumewe akadakia.

Mzee Mbegu akawatazama kwa zamu mtu na mkewe halafu akauliza "Kwa nini asirudi?"

Mama Vayajo akaangalia huku na huku kuona kama kuna mtu anasikiliza mazungumzo yao. Kumbuka walikuwa bado wodini. Walikuwa wanajiandaa kuondoka na mgonjwa aliyeruhusiwa. Lakini bado alikuwa amelala usingizi.

Alipoona hakuna mtu anayemuangalia akajibu "Kule ndiyo kuna wabaya wake, akirudi huyu anaweza kuumwa tena."

"Kuumwa tena na nyoka?" Mzee Mbegu akamuuliza mama mkwe wake.

"Hapana baba, ugonjwa unaweza kumrudia tena huyu." Akajibu.

"Mimi naona arudi tu kwa shangazi yake Morogoro." Baba wa mgonjwa akashauri, halafu akaongeza.

"Kwanza Kibaha si alikuja kwa muda tu? Arudi alikokuzoea."

"We baba Zulfa kwa hali hii. Yaani arudi Morogoro. Thubutu, labda mimi siyo mama yake. Mpaka nihakikishe mwanangu amepona kabisa."

Wote wakashtuka kwa msimamo wa mama huyo. Halafu ni kama macho yao yakawa yanamuuliza "Sasa unataka akakae wapi?"

"Nataka akaishi sehemu ambayo si mbali sana na nyumbani ili nipate hata nafasi ya mimi mwenyewe kumtazama mara kwa mara." Akajibu kana kwamba na yeye alijua swali atakaloulizwa baadaye.

"Wazazi wangu hebu naomba na mimi niongee. Samahani sana. Mimi nimejitolea tu matibabu na kila kitu, lakini sina mamlaka yoyote yale. Lakini naona nitoe ushauri tu."

"Sema tu mwanangu usiwe na wasiwasi." Alisema Baba Zulfa. Mpaka kufikia hatua hiyo, tayari Jerry alikuwa amejijengea heshima kubwa kwao. Kitendo cha kukimbiwa na mke siku ya harusi, lakini bado amekuwa karibu na familia katika kipindi cha kumuuguza shemeji yake, huku akijitolea gharama za matibabu, zilimfanya kukubalika mara dufu.

"Naomba kama itawapendeza Zulfa akae kwangu kwa muda wakati anarudisha afya yake."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# MAISHA MANASE AFUNGA MWAKA KIAINA

MWIMBAJI nyota wa Injili anayeishi Marekani, Maisha Manase, ameibuka kivingine na wimbo 'I Love You Everyday' baada ya kukaa kimya kwa muda mrefu.

Akizungumza na gazeti hili, Manase amesema anafahamu Tanzania ana mashabiki wengi ndio maana wamekuwa wakiulizia kazi mpya kutoka kwake hivyo ngoma hiyo ambayo ameiachia juzi itawabariki wengi.

"Tunapaswa kurudisha upendo wa Mungu kwake kila siku ndio maana katika majira haya ya mwisho wa mwaka nimeamua kutoa wimbo huu 'I Love You Everyday' ili Mungu aendelee kutukuzwa," amesema Maisha.



## Chid Benzi akana kumiliki wahuni

BIFU kati ya mtayarishaji wa muziki nchini, Mr T Touch na rapa Chidi Benz limechukua sura mpya, baada ya mwanamuziki huyo kusema tuhuma anazopewa za kutaka kumdhuru yawezekana amemfananisha.

Mr T Touch juzi alitoa waraka mrefu ambao ulimtuhumu Chid Benzi kwa kutaka kumdhuru akitumia genge lake la wahuni na kufanya majaribio kadhaa ya kumuumiza.

Chidi Benzi, amesema kwamba anachokisema mtayarishaji huyo ni kama amemfananisha kwani yeye sio mtu wakumfuata mtu na genge.

Amesema kama kupishana huwa inatokea lakini sio kufuatana na magenge ya wahuni.

"Kachanganya tu hakuna kitu chochote mimi na yeye, kama ni kuomba pesa na akakataa nikaanza kumfuatilia nyuma basi itakuwa ni wasanii wote, yeye kachanganya tu tofauti kabisa mimi sikua Sinza na kuhusu genge mimi natembea peke yangu, pia nakaa peke yangu Ilala" amesema

Ameongeza "Sina genge la kihuni mimi kama nataka kumfanyia mtu miyeyusho ambaye kaniletea miyeyusho namfuata mimi mwenyewe, sina hata haja ya genge na siwezi kumtafutia mtu matatizo kwa hiyo inawezekana kazingua au kafananisha "

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DAPAY NA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imefanya mazungumzo juu ya kumsajili tena mchezaji wao wa zamani raia wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28, ambaye klabu yake ya sasa Barcelona ipo tayari kusitisha mkataba wake. (***Sky Germany***)

### ENDRICK AWINDWA

CHELSEA na Real Madrid bado zipo katika mbio za kutaka kuinasa saini ya mshambuliaji kinda wa klabu ya Palmeiras Mbrazili Endrick licha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 16 kutakiwa Paris St-Germain. (***Fabrizio Romano***)

### WINKS KUSITISHIWA

KLABU ya Sampdoria ya Italia huenda ikasitisha mapema mkataba wa mkopo wa kiungo raia wa England, Harry Winks anayemilikiwa na klabu ya Tottenham Hotspur. Winks mwenye umri wa miaka 26 yupo katika mkopo wa mwaka mzima na Sampdoria lakini hajaichezea hata mechi moja klabu hiyo kutokana na majeraha ya kifundo cha mguu. (***Calciomercato)***

### IWOBI MKATABA MPYA

KIUNGO raia wa Nigeria, Alex Iwobi mwenye umri wa miaka 26 yupo mbioni kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu na nusu na klabu yake ya Everton utakaompatia mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. (***Sun)***

### MINA KUACHIWA

KLABU ya Everton pia ipo tayari kuwaachia beki wa kati, Yerry Mina mwenye umri wa miaka 28 na kiungo raia wa Mali, Abdoulaye Doucoure mwenye miaka 29, endapo watapata klabu za kuwasajili katika dirisha la usajili la Januari. (***GiveMeSport***)

### EPL KUTOTUMIA MFUMO

LIGI Kuu ya England, EPL, haitatumia mwongozo mpya mkali wa Shirikisho la soka la kimataifa, Fifa, juu ya dakika za majeruhi ambao umezifanya baadhi ya mechi katika Kombe la Dunia linaloendelea nchini Qatar kuchezwa mpaka kwa dakika 100. (***Mail)***

### DIABY APIGIWA HESABU

KLABU ya Manchester United inapiga hesabu za kumnyakua mshambuliaji raia wa Ufaransa anayechezea klabu ya Bayer Leverkusen, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 23. (***Fichajes)***

### ORTEGA KUTOINUNUA MAN

BILIONEA Amancio Ortega, ambaye ni mmiliki wa maduka maarufu ya nguo na mitindo ya Zara hana mpango wa kuinunua klabu ya Manchester United licha ya ripoti za awali kumhusisha tajiri huyo mwenye miaka 86 na ununuzi huo. (***Cadena Cope***)

### BUSQUETS AONGEZEWE

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez ameutaka uongozi wa klabu hiyo kumuongezea mkataba wa mwaka mmoja kiungo mkabaji raia wa Hispania, Sergio Busquets mwenye miaka 34. (***Sport***)

### TOURE KUINOA WIGAN

MLINZI wa zamani wa Arsenal na Manchester City, Kolo Toure mwenye umri wa miaka 41 ameingia makubaliano ya miaka mitatu na nusu kuwa kocha wa klabu inayoshiriki ligi ya Championship ya Wigan. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR KUKOSA MECHI MBILI QATAR

**●●● Ni baada ya kuumia kifundo cha mguu kwenye mchezo wa ushindi kwa Serbia...**

**DOHA,** Qatar

NEYMAR atakosa mechi mbili zijazo za Brazil za Kombe la Dunia baada ya kupata jeraha la mguu wa kulia, amesema daktari wa timu hiyo.

Mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 30 aliondolewa uwanjani dakika ya 80 ya mchezo wa siku ya Alhamisi ambapo Brazil waliichapa Serbia 2-0 baada ya kugongana na Nikola Milenkovic. Neymar alionekana kuwa mwenye huzuni wakati alipokuwa akipata matibabu na picha zilionesha kifundo chake cha mguu wa kulia likiwa limevimba.

**Neymar alivua kiatu chake kuonesha mguu wa kulia uliovimba vibaya baada ya kuon dolewa uwanjani mwis honi mwa mchezo huo.**

Alilielezea jeraha lake kama 'moja ya nyakati ngumu zaidi katika kazi yangu'.

"Nimejeruhiwa, ndiyo sio vizuri, itaniumiza lakini nina uhakika nitakuwa na fursa ya kurejea tena uwanjani," alisema Neymar.

"Nitafanya kila niwezalo kusaidia nchi yangu, timu yangu na mimi mwenyewe.

Kukosekana kwake kutamfanya Gabriel Jesus, Antony au Gabriel Martinelli kuanza kwenye kikosi cha kwanza , Tite dhidi ya Uswisi.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
SPAIN
VERSUS
GERMANY
1 | 2.33
X | 3.51
2 | 2.81

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GAKPO KUTIKISA USAJILI JANUARI

**DOHA,** Qatar

CODY Gakpo wa PSV amekuwa mmoja wa nyota waliochipukia mapema katika Kombe la Dunia, na inasemekana atawaniwa na baadhi ya Klabu kubwa duniani Januari.

Gakpo mwenye umri wa miaka 23 ametumia maisha yake yote akiwa na PSV baada ya kufika katika akademi yao ya vijana mwaka 2007, na amepanda na kuwa mmoja wa washambuliaji wakuu wa Uholanzi.

Amefunga mabao tisa na kusaidia mengine 12 katika mechi 14 za kwanza za Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, na ameanza msimu wa Kombe la Dunia kwa mabao katika kila mechi kati ya mbili za kwanza za hatua ya makundi dhidi ya Senegal na Ecuador.

Akiwa amehusishwa na Leeds United kabla ya msimu huu, inasemekana aliamua kubaki na PSV ili kuhamia klabu kubwa zaidi - na sasa timu zilizopo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya zinamuwania.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa Uholanzi, Marco Timmer, klabu zitakazofanya jaribio la kumsajili mchezaji huyo ni pamoja na Liverpool, Real Madrid, Bayern Munich na Manchester United.

Baada ya kusema hapo awali angefurahi kusalia Uholanzi hadi mwisho wa msimu kabla ya kuhamia Ligi Kuu ya England, thamani ya Gakpo inasemekana kupanda zaidi ya pauni milioni 50 kwa sasa.

Kulikuwa na ripoti mapema msimu huu kwamba hali ya kifedha ya PSV ingewalazimisha kukubali zabuni zaidi ya karibu pauni milioni 30.

Hata hivyo, sasa inaonekana kwamba atakuwa na thamani ya fedha kubwa zaidi Januari.

# Kane: England bado ina nafasi kombe la Dunia

**DOHA,** Qatar

HARRY Kane amesisitiza kuwa matokeo ya England dhidi ya Marekani "sio mwisho wa dunia kwetu" na anaiweka timu katika nafasi nzuri huko Qatar.

Nahodha Kane alikosa nafasi dakika za lala salama baadaya mpira wake wa kichwa kwenda nje huku mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Al Bayt ukimaliza kwa sare.

Marekani walikuwa timu bora kwa sehemu kubwa za mchezo, lakini England waliimarika katika hatua za mwisho.

"Haukuwa utendaji wetu bora, kwa hakika," alisema Kane akiiambia ITV.

"Tulikuwa na vipindi vizuri na mpira na kutengeneza nafasi nzuri, lakini hatukuwa na matokeo ya mwisho leo (juzi).

"Ni safu safi sana, inatuweka katika nafasi nzuri kwenye kundi."

Baada ya ushindi wa 6-2 wa ufunguzi dhidi ya Iran, matarajio kwa Englan walipanda kiwango, lakini wakashindwa kupata ushindi.

"Ilikuwa tofauti kabisa na mchezo dhidi ya Iran, ambapo tulichukua nafasi zetu vizuri," alisema Kane, kabla ya kuwapongeza Wamarekani.

"Angalia, kwa ujumla wao ni timu ngumu, na tutasonga mbele. Walitubana sana na kufanya iwe ngumu kwetu. Nilidhani wakati fulani tulikabiliana nayo vizuri, ni timu nzuri na lazima tuipe heshima hiyo.

"Sare sio mwisho wa dunia kwetu. Tunajua tunaweza kucheza vizuri zaidi ya hapo, lakini ni sare katika Kombe la Dunia, hakuna mchezo rahisi katika Kombe la Dunia."



HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# AZAM KAZI MOJA KWA COASTAL UNION LEO

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Azam FC kinashuka dimbani leo kulipa kisasi na kusaka heshima mbele ya wenyeji wao Coastal Union katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Azam itakuwa wenyeji wa Coastal Union katika dimba la Azam Complex, uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Wanalambalamba hao wanashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kuondolewa Coastal Union katika nusu fainali ya michuano ya kombe la Shirikisho la Shirikisho la Soka Tanzania (FA) msimu uliopita.

Leo kikosi cha Azam kitakuwa na mabadiliko madogo kwa wachezaji wake baada ya kurejea kikosini kwa nyota wake Selemani Sopu baada ya kutoka katika majeraha.

Sopu ambaye msimu uliopita aliitumikia Coastal na kuwa miongoni mwa kikosi ambacho kiliwaondoa Azam katika michuano hiyo sasa anawatumikia waajiri wake wapya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Azam, Kalimangonga Ongala amesema kikosi kipo tayari kwa ajili ya kukabiliana na wapinzani wao kuhakikisha wanaendelea kukusanya pointi tatu muhimu katika mchezo huo na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu na ushindani mkubwa kwa sababu pande zote mbili zinahitaji kupata matokeo mazuri kila mmoja akisaka pointi muhimu ili kufikia malengo yao.

"Mechi hii itakuwa ya heshima na kisasi kwa sababu msimu uliopita Coastal Union walitutoa katika mashindano lakini hatuwezi kwenda na historia hiyo kwa sababu hii ni ligi na tumefanya maandalizi mazuri kutafuta matokeo chanya," alisema Ongala.

Aliongeza; "tunawaheshimu wapinzani wetu Coastal kwa sababu wana wachezaji wazuri pamoja na benchi imara kwa kubadilisha kocha, ni nina imani hautakuwa mchezo rahisi kwa pande zote."

Azam FC mwaka huu wamedhamiria kusaka pointi kila mechi na kutorudia makosa ya msimu uliopita na sasa wakihitaji kushika nafasi ya kwanza katika msimamo wakivutwa shati na Yanga wote wakiwa na pointi 29 katika msimamo.



Mchezaji wa timu ya Dar City, Baraka Shabani (kushoto), akimiliki mpira mbele ya mchezaji wa TRA, katika mchezo wa ligi daraja la pili uliopigwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba hasira zote kwa Polisi

INATOKA UK. 24

wa nyumbani ikiwa kwenye nafasi ya 14, mechi 13 na pointi tisa, hivyo itataka kutoka kwenye eneo hatari la msimamo.

Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, John Tamba amesema wataingia na staili tofauti kwenye mechi ya leo.

"Tuna masaa machache kabla ya kucheza na Simba, sisi tumejiandaa vizuri, tunatarajia kutoa ushindani na kuzisaka pointi tatu kwenye uwanja wetu wa nyumbani," alisema.

"Najua kila kitu kitabadilika, tulikuwa tunatumia uwanja wa Sheikh Amri Abeid, ule haukuwa uwanja wetu kamili wa nyumbani, nina uhakika sasa mashabiki wetu watakuja kwa wingi," alisema kocha huyo.

## Mayele msimu huu hataki mzaha

INATOKA UK. 24

makubwa zaidi hasa kusaidia timu yake na kuhakikisha anatumia vema nafasi wanazotengeneza ili kufunga idadi kubwa ya mabao kwa ajili ya kujiweka katika nafasi nzuri mwisho wa msimu katika ufungaji.

"Nataka kuendelea kuongoza kwenye ufungaji, huku pia naipambania timu kupata matokeo mazuri," alisema Mayele.

Alisema malengo makubwa msimu huu ni kutetea taji lao la ubingwa wa Ligi Kuu.

Mayele aliongeza kusema amejipanga kupambania timu kwa kujituma na kuhakikisha anafunga ili aweze kutwaa kiatu cha dhahabu mwishoni mwa msimu huu.

Mshambuliaji huyo msimu uliopita alikosa tuzo ya ufungaji bora akishika nafasi ya pili akiwa na mabao 16 nyuma ya aliyeibuka kuwa kinara George Mpole aliyetikisa nyavu mara 17..

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 27/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1096 | Japan vs Costa Rica | 1.45 | 4.18 | 6.97 |
| 14:00 | 1545 | Dinamo Moscow vs Gazovik Orenburg | 1.88 | 3.60 | 3.45 |
| 14:00 | 1712 | Rostov vs Akhmat Grozny | 2.27 | 3.50 | 2.67 |
| 14:00 | 5002 | Kariobangi Sharks vs Ulinzi Stars | 2.67 | 2.67 | 2.86 |
| 14:00 | 5361 | Buducnost vs Jezero | 1.76 | 3.41 | 4.19 |
| 14:30 | 2845 | Reggina vs Benevento | 1.88 | 3.31 | 4.06 |
| 15:00 | 1021 | Akron Tolyatti vs Ska Energiya | 2.52 | 3.05 | 2.66 |
| 15:00 | 1240 | Shkendija vs FK Tikves Kavadarci | 1.70 | 3.31 | 4.76 |
| 15:00 | 2107 | Neftchi Baku vs Sabayil | 1.23 | 5.46 | 9.75 |
| 15:00 | 4198 | Zorya Lugansk vs FC Minaj | 1.43 | 4.28 | 6.02 |
| 15:00 | 4483 | Rubin Kazan vs Neftekhimik | 1.55 | 3.80 | 5.26 |
| 15:00 | 4708 | Tusker vs Nairobi City Stars FC | 1.84 | 3.15 | 4.17 |
| 15:30 | 2854 | Ebbsfleet vs Fleetwood Town | 2.91 | 3.41 | 2.23 |
| 16:00 | 2198 | Belgium vs Morocco | 1.92 | 3.39 | 3.94 |
| 16:00 | 2243 | Urozhay Krasnodar vs Volga Ulyanovsk | 2.15 | 3.01 | 3.30 |
| 16:00 | 3180 | Kryliya Sovetov vs Fakel | 1.34 | 4.68 | 7.02 |
| 16:00 | 4909 | Polisi Tanzania vs Simba | 6.82 | 3.99 | 1.42 |
| 16:00 | 5082 | Burgos vs Zaragoza | 2.53 | 2.83 | 3.02 |
| 16:00 | 5947 | Zenit St Petersburg vs Spartak Moscow | 1.55 | 4.18 | 4.67 |
| 16:30 | 4676 | Crotone vs Latina | 1.68 | 3.54 | 5.18 |
| 17:00 | 2320 | Brescia vs Spal | 1.89 | 3.37 | 3.92 |
| 17:00 | 2346 | Cittadella vs Cosenza | 1.64 | 3.51 | 5.35 |
| 17:00 | 2483 | Frosinone vs Cagliari | 2.03 | 3.17 | 3.67 |
| 17:00 | 3273 | Sudtirol vs Ascoli | 2.37 | 3.11 | 2.97 |
| 17:00 | 4072 | Perugia vs Genoa | 3.86 | 3.27 | 1.94 |
| 17:00 | 4130 | Burton vs Chippenham Town | 1.35 | 4.95 | 7.13 |
| 17:00 | 4371 | Como vs Bari | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 17:00 | 5393 | Bristol Rovers vs Boreham Wood | 1.57 | 3.95 | 5.13 |
| 18:00 | 1580 | Gil Vicente vs Nacional Madeira | 1.73 | 3.46 | 4.28 |
| 18:00 | 2068 | National Bank vs Pyramids | 4.27 | 3.40 | 1.75 |
| 18:00 | 2310 | Apoel Nicosia vs Omonia Nicosia | 2.04 | 3.31 | 3.61 |
| 18:00 | 2957 | Al Ahly Cairo vs Arab Contractors | 1.61 | 3.62 | 4.89 |
| 18:00 | 4404 | Leganes vs Granada | 2.53 | 2.92 | 2.92 |
| 18:15 | 3314 | Newport vs Derby | 3.64 | 3.45 | 1.92 |
| 18:15 | 4951 | Lugo vs Levante | 3.52 | 3.12 | 2.10 |
| 18:30 | 2485 | Lausanne-Sport vs FC Aarau | 1.83 | 3.78 | 3.44 |
| 18:30 | 4258 | RS Waasland Beveren vs Lommel United | 1.51 | 4.54 | 4.94 |
| 18:35 | 5101 | Al Kuwait SC vs AL Qadsia | 2.06 | 3.35 | 3.16 |
| 19:00 | 1255 | FC Krasnodar vs FK Khimki | 1.33 | 4.68 | 7.60 |
| 19:00 | 1455 | Azam vs Coastal Union | 1.42 | 3.98 | 6.99 |
| 19:00 | 2315 | Lokomotiv Moscow vs Nizhny Novgorod | 1.97 | 3.45 | 3.30 |
| 19:00 | 4205 | Goeztepe vs Altay | 1.82 | 3.41 | 3.89 |
| 19:00 | 5790 | Croatia vs Canada | 2.13 | 3.25 | 3.40 |
| 20:00 | 2180 | AEL Limassol vs Anorthosis Famagusta | 2.44 | 3.21 | 2.86 |
| 20:00 | 2803 | FC Cartagena vs Eibar | 2.37 | 2.97 | 3.12 |
| 20:00 | 3773 | Ipswich vs Buxton FC | 1.14 | 7.31 | 14.81 |
| 20:00 | 5435 | Palermo vs Venezia | 2.38 | 3.22 | 2.87 |
| 20:00 | 5674 | Moreirense vs CF Estrela | 1.66 | 3.75 | 5.00 |
| 22:00 | 2889 | Spain vs Germany | 2.33 | 3.51 | 2.81 |
| 23:45 | 4287 | Boavista vs Vilafranquense | 1.80 | 3.35 | 4.08 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Novemba 27, 2022

Nipashe




Neymar kukosa mechi mbili UKURASA 21



Nyota wa Simba, Augustine Okrah na Clatous Chama wakiwa kwenye mazoezi kujiandaa na mchezo dhidi ya Polisi. **PICHA:SIMBA**

## Mayele msimu huu hataki mzaha

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI na kinara wa mabao wa Yanga, Fiston Mayele ambaye amerejea katika ubora wake wa kuzifumania nyavu amewaahidi mashabiki kuendelea kupambana kwa ajili ya kuisaidia timu kupata matokeo mazuri katika michezo yao yote iliyopo mbele ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga imeendelea kufanya vizuri huku ikiwa haijapoteza mechi 48 na wakiongoza msimamo kwa pointi 29 kabla ya mechi ya jana Jumamosi dhidi ya Mbeya City.

Mbali na Yanga kuongoza msimamo lakini pia nyota huyo naye ni kinara wa mabao ndani ya ligi hiyo akiwa ametikisa nyavu mara nane kabla ya mchezo wa jana.

Akizungumza na gazeti hili, Mayele alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa na ana imani wataendelea kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika kila mechi na yeye akiendelea kutikisa nyavu ili kufikia malengo yao.

Alisema anatarajia kufanya

INAENDELEA UK. 23

# SIMBA HASIRA ZOTE KWA POLISI

## Yasaka pointi, heshima na kurudi kwenye mbio za ubingwa Ligi Kuu huku...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya Jumatano iliyopita dhidi ya Mbeya City na kuzua malalamiko makubwa kutoka kwa wanachama na mashabiki wao, timu ya Simba leo itakuwa tena ugenini kwenye Uwanja wa Ushirika Moshi mkoani Kilimanjaro kujaribu bahati yake dhidi ya wenyeji Polisi Tanzania.

**Utakuwa ni mtihani mwingine kwa Simba ambayo inaonekana ni nyanya ikicheza kwenye viwanja vya ugenini tofauti na Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Itakuwa ni mechi ya raundi ya 14 ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo inahitaji ushindi ili kufikisha pointi 28, kwa ajili ya kuweka hai matumaini ya kuwania ubingwa wa Tanzania Bara ambao ilinyang'anywa msimu uliopita na watani zao wa jadi, Yanga.

Kaimu Kocha Mkuu wa timu, Juma Mgunda amesema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na anatarajia mechi itakuwa ngumu bila kujali matokeo mabaya ambayo Polisi inayapitia.

"Kubwa ni kwamba tumefika salama, na maandalizi ya kucheza mchezo mzuri na mgumu yamekamilika na tuko tayari kushindana na wenzetu, tunaiheshimu Polisi ni timu nzuri na timu yenye upinzani," alisema Mgunda.

"Vijana wangu wanaelewa wanakwenda kucheza mechi ya aina gani. Nimekuja na wachezaji 22 na wote wapo fiti na tunajua ni mechi ambayo tunahitaji matokeo, unapokwenda kushindana na mpinzani wako kwenye ligi haijalishi yupo kwenye nafasi gani au hali waliyokuwa nayo na pointi walizonazo," aliongeza.

Kuhusu maneno ambayo wamekuwa wakitupiwa na wanachama na mashabiki wa Simba kutokana na kufanya vibaya, alisema hiyo wanaichukulia ni changamoto tu na hayakwepeki kwenye mpira.

"Maneno kwenye mpira hayakwepeki, kuna wanaojua mpira, na kuna wanaotaka matokeo tu, vitu hivyo havikwepeki na huwezi kuwakwepa, ni sehemu ya jamii ya mpira, wachezaji wangu wanaoambiwa moja, mbili, tatu, ni jukumu langu kukaa nao na kuwajenga kisaikolojia, kuwatayarisha, hata wao wanafahamu usipofanya vizuri lazima kutakuwa na presha ya watu kwa ajili ya kufanya vizuri, na mara nyingi changamoto huwa haikimbiwi, unaikabili," alisema.

Polisi Tanzania itacheza kwa mara ya kwanza msimu huu kwenye uwanja wake

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >